Chapisho la 1 - 2020

Jukwa la Feminist Republik

# DZUWA





# NENO KUHUSU JARIDA LA FEMINIST REPUBLIK

Jarida la *Dzuwa* ni chapisho la mtandaoni ambalo hujumuisha simulizi zinazoegemea masuala ya Afrika na ambazo zinachunguza kwa kina tandu zinazounganisha uelewa na kushiriki utunzaji wa kibinafsi na ule wa pamoja, uponyaji na maarifa na matendo ya kiasili. Chapisho hili linaletwa kwenu na jukwa la Feminist Republik (ambalo kirasmi linajulikana kama kama Jukwaa la Watetezi Haki za Kibinadamu za Wanawake wa Afrika). Ni mpango wa shirika la Urgent Action Fund – Afrika ambao una uhuru wa kihariri.

Hamu yetu kuu ni kukusanya hifadhi yenye utajiri mkubwa ambayo itawakuwa yenye manufaa mengi kwa watetezi wa kifeministi barani Afrika kwa kuweza kuteka na hata kutoa usambazaji thabiti wa njia na ujuzi mbalimbali kuhusu uponyaji na hali bora, yote yakinuia kuimarisha na kuunga mkono safari zao za kibinafsi, kifamilia na kijamii za uponyaji na ustawi.

Michango hii iliyoko kwenye toleo hili la jarida ni haswa sauti na kujieleza kwa watetezi wa Afrika, waponyaji, watetezi wa kisanii, waratibu, wasomi, wanamuziki na wengine wengi waliojituma katika kazi za haki za kibinadamu na haki za kisheria. Ni kupitia kwa kitendo hiki cha kisiasa cha kufanya makusudi ya kutoa heshima, kutambua, kuelewa na kukumbana na maumivu yetu ya pamoja ndilo litatupatia fursa ya kupata uponyaji. Tunanuia pia kuitumia nafasi hii kuweza kupata fursa ya kuchota ujuzi na urithi tulioukuza sisi wenyewe kama kisima muhimu cha ukakamavu na busara.

Sisi pia tuna furaha kuu ya kuandaa safari ya bara zima tukiandamana pamoja na wewe kwenye ziara yenye mada yetu kuhusu wakati wa mzuko wa shida. Hili toleo la kwanza kabisa la jarida hili pia ni muhimu sana kwa sababu tutakuwa tunakujulisha kuhusu chimbuko la jarida la Feminist Republik ikiwa ni pamoja na vipengee muhimu kutoka kwenye uanzilishi rasmi na tafrija mnamo Desemba 2019 mjini Naivasha, Kenya.

Toleo hili lina mafunzo kuhusu dhana na uzoefu wa wale waliochangia huku tukipitia kwa ujasiri janga ambalo limeunasa ulimwengu wote. Kupitia kwa janga hili tunaweza kupata taswira ya yale tuliyoyafahamu muda wote huu; ya kwamba wale waliothirika vibaya zaidi ni wale tu ambao pia wanakumbana na kutokuwepo usawa, na hili ni tokeo la kusikitisha ila ambalo silo la kushangaza.

Haya yote ni kwa sababu bado tunaishi katika mfumo wa dunia ambao umepuuza mizizi yake iliyotokana na kuwajali kwa kina watu wake wote, na badala yake umetekwa na kutawaliwa na ajenda za kuongezeka kwa uongozi wa kimabavu, ubepari, mifumo yaya huria mamboleo na ubeberu. Miongoni mwa yale tuliyowaandalia kwenye toleo hili ni pamoja na uchambuzi wa anuwai za mihemko, uzoefu na kujieleza ambako kunajitokeza kama tafakari sahihi ya safari tuliyoikamilisha, safari ambayo ingalipo mbele yetu na, ila muhimu zaidi, jinsi ambavyo tuna ukakamavu ya kuweza kukumbana na mawimbi ya ugandamizaji na ubaguzi.

Kila toleo la jarida letu litakuwa na mhariri mgeni wa ambaye atakuwa ndiye rubani mwenye jukumu la kutuongoza kwa kuzingatia ari na hekima kutoka pembe mbalimbali za bara hili tukufu. Toleo hili la kwanza halitakuwa tofauti, mhariri wetu mgeni ni Solome Nakaweesi, mfeministi kutoka Uganda mwenye tajriba kuu ya kupenda bara la Afrika. Anashiriki nasi mawazo yake na uzoefu katika kuhariri michango mbalimbali iliyojumuishwa kwenye toleo hili la kwanza kabisa la jarida. Hebu furahia toleo letu la kwanza la Dzuwa!

Peperusha maoni
yako na habari kwa feministrepublik@uaf-africa.org

**Melissa Wainaina**
**Feminist Republik Creative Facilitator**



# Wigo wa Mhemko na Hisia..

FAHARASA KUTOKA KWA MHARIRI WETU MGENI
SOLOME NAKAWEESI

# DZUWA! ALFAJIRI MPYA!

DZUWA! Alfajiri mpya iko hapa! Safari mpya yenye msisimko tunaianza, jarida la kwanza la Dzuwa... Kuibuka kutoka Mashariki kama vile Jua linaloibuka basi litazuru na kupitia sehemu zote za Bara hili Kuu la Afrika! Inaambatana na matamanio, ndoto, nguvu za watetezi wetu wa kike shupavu wa haki za binadamu wa Kiafrika. Kutokana na ndoto zetu za asili zilizoanzia kule Lagos, kuzitekeleza huko Naivasha na zaidi, na sasa tunayo Dzuwa. Sio kwa bahati kwamba Dzuwa iko hapa wakati Afrika na Ulimwengu kwa ujumla wanatafuta majibu suluhisho mpya kwa matatizo ya zamani... kuongea juu ya uwezekano wa 'Mtindo Mpya Ulimwenguni' baada ya janga la COVID-19 na shida zingine nyingi, shida na ukosefu wa usawa ambao ulizua kujipata hapa tulipo sasa. Watetezi Wanawake wa haki za binaadamu wa Kiafrika, wametumia miongo kadhaa na karne kupambana dhidi ya ukali na uharibifu wa mfumodume kwani inazuilia, na kwa vile unaimarishwa na aina nyingine za ukandamizaji kama - ubaguzi wa rangi, huria, huria mamboleo, uharamishaji wa ujinsia, kupuuzwa kwa wasiojiweza, ubaguzi unaotegemea umri, ubeberu, ubepari, udikteta na ukandamizwaji wa serikali, na mengine mengi! Na, bila shaka kutekeleza haya yote kwa bidii kumetuwacha bila nguvu kabisaa, kutuacha hoi kabisaa ila wakati huo huo kutuwezesha kutambua kuwa lazima tujipange upya kama kielezo cha wakala wetu na uongozi - lazima tujishughulishe kujitunza sisi wenyewe na dada wengine na wandugu.

Hakuna kuhoji kuwa maisha ya wanawake watetezi wa haki za binadamu yapo hatarini, afya mbaya, kukosa usingizi, hasira, unyogovu na uchovu – yote ni kweli na kwamba hili sio jambo jipya – Suala ambalo ni jipya ni kwamba kujitunza, ustawi na haki ya uponyaji yameibuka na kuweza kuonekana zaidi na sisi tunayachukulia haya kwa ujasiri.

Jambo ambalo ni jipya ni kusudi letu eti kwamba ni lazima tufichukue hatua kuhusu ustawi wetu kama watu binafsi na hata kwa umoja.

Kilicho kipya ni ushujaa ambao tunajituma nao upya na ambao tunaamka nao kila siku ili kupingana na ukandamizaji uliokithiri pembe zote dhidi ya shinikizo letu, kupinga hali inayochukuliwa kuwa ya kawaida, kuunda utaratibu mpya wa ulimwengu ila kwa wakati huo huo tunatekeleza makusudi ya kujitunza sisi wenyewe - kuwa na ujasiri kuhusu uhatarishi wetu na kunyakua fursa ya kujitetea! Kile kipya ni kwamba tumekusanyika pamoja kama muungano muhimu ili kuchanga uwezo wetu wa pamoja, nguvu, ujuzi, mitandao na maono ili kuhakikishia ulimwengu bora zaidi kwa wanawake watetezi wa haki za binadamu wa Kiafrika katika anuwai yetu - wanawake, wabadili jinsia, wasiokubali kuambatanishwa na jinsia yoyote – wote ambao ni watetezi wa haki za kibinadamu ili kushiriki, kujiondolea dhiki, kubuni kwa pamoja, kutoa hasira, kulia, kusherehekea na zaidi ya yote, kuwa sisi tu!

Kama harakati za wanawake na watetezi barani Afrika, itikadi zetu na uundaji wa pamoja wa 'Mfumo Mpya Ulimwenguni' ulianza muda mrefu uliopita – mbali kabla ya COVID-19. Na wasanii wakisumbua na kuvuruga vikoa vya kimwili na kidijitali kwa kutumia sanaa yao; wafikiriaji wabunifu wakiangazia mada mbadala ambazo huvuruga maoni ya kawaida kuhusu miili, jinsia na ujinsia kupitia ushairi, nyimbo, densi au ngonjera; wanaharakati wakisukuma mipaka juu ya haki za wanawake katika anuwai zao, wasomi wakijadiliana na kuunda dhana mbadala kuhusu za kifeministi, na wanawake wa Kiafrika wakiamka kila siku ya maisha yao kukuza jamii, harakati za kijamii na bara hili lenye urembo – bila hata kujali ya kwamba ni nadra kutambuliwa. Haya yote huhitaji kujitolea kwetu kama watu binafsi, kwa pamoja, kama harakati na hata mashirika.

# DZUWA! ALFAJIRI MPYA!

Hii yote inaangazia ukweli kwamba ikiwa tutaweza kuendeleza kile tunachofanya, ni lazima tujitunze kama watu kila mmoja binafsi na pia kwa pamoja; lazima tuwekeze katika kubuni na kushiriki njia hizi tofauti ambazo uponyaji na utunzaji hufanywa; lazima tuunde wakati na rasilimali kwa sisi; lazima tujiweke kwa mara nyingine tena sisi wenyewe kama kipaumbele na kama sehemu ya mfumo mpya wa ulimwengu — na wala sio kusudi la ubinafsi - ni Mfumo Mpya wa Ulimwengu! Mfumo huu mpya ni sharti ushughulikie Dhulma dhidi za Ustawi wa Wafemiinisti.

Ustahimilivu wetu kama wanawake watetezi wa haki za binadamu wa Kiafrika sio tu kupitia kwa ile kazi tunayoifanya, lakini pia kupitia jinsi ambavyo tunajiinua tena na kuibuka kila tunapoanguka. Ndiyo sisi ni baadhi ya walio hatarini, lakini pia sisi tuna ukakamavu. Sisi ni wenye kupatana kwa urahisi, ila pia ndo nguzo zenye nguvu ndani ya jamii zetu, mishikamano yetu, mashirika na Bara la Afrika. Tuna utofauti utofauti, ndiyo, ila kutokana na utofauti huo kama wanawake watetezi wa haki za binadamu wa Kiafrika tunapata minyororo yenye nguvu ambayo inatufunga pamoja. Ustahimilivu wetu ni pamoja na sisi kuutambua kwa jina, kushiriki hadithi zetu, na kamwe kutoacha kuwa na wasiwasi - Na hii ndivyo toleo la kwanza lilivyo — lenye anuai ya utofauti, imara, lisilokuwa na utulivu lakini bado linazungumzia hali yetu halisi, kuvunja miiko ya unyamavu na kuunganisha upekee wetu kama viongozi, wasanii wa viongozi , wafikiriaji wa ubunifu, waandishi, viongozi. Inavuruga maoni ya kawaida kuhusu imani, dini, miili, jinsia, uwezo, imani na ujinsia - ndio unaibua ndani yetu madai ya kifeministi! Je! Ni utamu ulioje kuwa katika hali ya kubabaika na huku tumechokorwa manyoya yetu?

Toleo la Uzinduzi la Dzuwa linakuletea mada nyingi mbalimbali za kukuchochea utafakari na hata kukufanya usisikitike — Bila shaka ufeministi ni wa kukupunguzia starehe.

Masuala kuanzia imani hadi ujinsia, kupambana na serikali za kukandamiza, hadi kunawiri hata kwenye janga la COVID-19, kushiriki njia za uponyaji, kusawazisha vielezo vyetu na ibada zetu za kiroho (kama vile kusawazisha Ukristo na mazoea ya uponyaji wa Kiasili) hadi kwa afya ya akili na kuchanganua masuala ya COVID-19 kutoka kwa mitazamo ya jinsia. Uwasilishaji wa toleo la kwanza la Dzuwa ni kupitia utumiaji wa mashairi, sanaa, kujieleza kwa njia za ubunifu, vitendo vya ustawi, simulizi za hadithi, mahojiano, makala, yaliyolenga kuamsha moto ndani yako, lakini pia kwa wakati huo kukufanya usitulie starehe - ni kweli ya kuwa toleo hili lina kina cha ufeministi ila hiyo imeungwa na achari ya kejeli, vichekesho na hata fumbo ambalo litakupa fursa ya kujishindia baadhi ya tuzo - hakikisha umeshinda hii na tushirikiane kuendelea na mazungumzo. Hizi zote zimepangiliwa ili kujaza upya roho na kufufua mioyo ya wasomaji wetu.
Raia wa Feminist Republik, sio tu eti naona fahari kuu kwa heshima hii, lakini nimejinyenyekeza sana kwa kuwa Mhariri Mgeni wa toleo hili la Uzinduzi wa Jarida la Dzuwa. Ni matumaini yangu kuwa Toleo hili la kwanza la Dzuwa linafungua, kuwasha cheche, kuthibitisha na kuhalalisha kuthubutu kwako mwenyewe kama mtu binafsi na kule kwa pamoja, na kuunda upatanisho ili kupata marejesho, huruma na hatimaye njia za uponyaji. Natumai inachecheta kufikia viwango vya kutaka kuchangia hadithi zako mwenyewe za ushupavu, za kusawazisha utashi wako na ustawi, usemi wa kisanii na safari za uponyaji na utunzaji — tuna hamu kubwa sana tukisubiri mchango wako katika matoleo ya baadaye. Na kwa kweli, jisikie huru kutumia sehemu ya 'Barua kwa Mhariri' ili uweze kushiriki maoni na mawazo yako kuhusu ni nini kilikuvutia zaidi na kutoa mapendekezo kama ni mada zipi ungependelea kuona katika toleo letu lijalo.

Haya ni Mapinduzi, Karibu na Furahia Mapinduzi! Furahiya DZUWA!

**Solome Nakaweesi**
**Mfeministi Mtetea-Afrika / Mtaalam wa Kujitunza na Haki ya Uponyaji Uganda, Afrika Mashariki**

# HII SI HADITHI, NI UTABIRI

Neno kutoka Coumba Toure, Senegal katika ufunguzi wa tamasha la Feminist Republik

Hii si Hadithi, ni Utabiri....
....Kwa wale walio na hiari kuwa watoaji wa maisha, kwa wale wanaokubali kuwa waboreshaji wa maisha,
kwa wale wanaokubali kupumua maisha,
ukakamavu na matumaini kwa
wao wenyewe kama watu binafsi
na kwa wengine kwa pamoja,
kwa wale ambao ndio wanaojenga kesho.

Mangala Ba aliuumba ulimwengu na kusema kwa wao ya kwamba
nitawapa hali ya kuzingatia haki.
Hii siyo hadithi, wala huu sio utabiri.
Huu ni uyakinifu unavyoendelea kuumbwa, siyo ndoto.
Nilipewa jina ili niwe mwanamke.
Mimi ni mmoja wenu tu, mwenye kuleta uhai, yule mwenye kuyaboresha maisha.

Je, wewe ni nani?

Utabiri ulisema ya kwamba kutatokea wakati mmoja
ambapo watu watakuwa wamepoteza mkondo wao
Wanawake watakuwa wamechokeshwa na hali ya kuchoka,
watafanya juhudi za kuungana, wataamua kutekeleza
matendo muhimu kuhusu hali hiyo yao.
Mbona wewe upo hapa? Unajua ni kwa sababu gani.
Utabiri huo ulisema ya kwamba watu watakusanyika
kutoka pembe zote.....
Na sasa sote tupo hapa!”

# ULIMWENGU MZIMA WA YANAYOWEZEKANA

## UZINDUZI NA TAMASHA ZA JUKWA LA FEMINIST REPUBLIK

### 8-11 DISEMBA, 2019, NAIVASHA, KENYA

Melissa Wainaina

Ushairi maarufu wa Coumba unatutayarishia hali kwa yale tuakayotarajia, na kuleta ahadi na utazamiaji kwenye ukumbi ya kwamba kutakuwa na njia mpya ya kuishi, kufanya kazi, kusalimika na kunawiri kama watetezi wa haki za wanawake wa bara la Afrika.

Mnamo Disemba 2019 Uzinduzi na Tamasha za Feminist Republik ziliandaliwa mjini Naivasha, Kenya. Tamasha hiyo yenyewe ilikuwa ni tukio kubwa la nguvu – hakujawahi kutokea au kushuhudiwa tena tamasha nyingine kama hiyo kwa muda mrefu. Kwa kuyatumia maneno ya Ndana Tawamba, Mkurugenzi Mkuu wa shirika la Urgent Action Fund Africa (UAF-Africa) yaliweza kunakili jinsi ambavyo tukio hili lilikuwa la kustaajabisha na lenye nguvu.

> ***"Ulikuwa ni wakati muhimu sana. Wakati usiosahaulika kwa sababu ya jinsi ambavyo uliundwa, ambavyo ulidhaniwa na ambavyo ulitokea na kuendeshwa. Ile tu sababu ya kwamba hili lilikuwa ni jukwaa la bara zima la Afrika ambapo wanawake 315, waliobadili jinsia, na wasioambatana na jinsia yoyote – ila wote watetezi wa haki za kibinadamu, wawakilishi wa mashirika ya kupambania haki za kibinadamu, miungano, harakati ktoka zaidi ya mataifa 35 kukusanyika pamoja kwa mkutano lilikuwa lenyewe ni jambo lisilo la kawaida.."***

Kongamano lilikuwa na tafsiri ya lugha tano zinazotumika katika mikutano ya umoja wa Afrika, almaarufu African Union, na pia kuongezea na tafsiri ya lugha ya ishara. Kulikuwa na utofauti wa waliowakilishwa kutoka pembe zote na kila aina ya watu, iwe ni wale waliokuja kama washiriki, waliokuwa kwenye majopo mbalimbali au wale waliochukuwa hatamu za kuongoza baadhi ya vikao. Lilikuwa ni tukio la heshima kuu na la kujivunia kwa shirika la Urgent Action Fund – Afrika kuweza kuandaa tamasha kama hii ambao ilifana sana kwa sababu ya juhudi zilizofanikishwa na ushirikiano mkubwa. Hili lilihitaji kuweza kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana na kundi kubwa kabisa la washirika kutoka kote barani Afrika, ikiwa ni pamoja na wenye maarifa ya uponyaji, viongozi wa masuala ya kitamaduni, wenye kutoa tiba za ushauri nasaha, na hata wengine wengi ambao ni wataalamu wa masuala mengine mengi mbalimbali yanayohusu malengo na dhamira mbalimbali ya kongamano letu. Baraza hilo lilikuwa na washiriki kutoka matabaka mbalimbali kwa kuzingatia umri au vizazi, yenye ujasiri na ukwasi mkubwa, yenye kuchanganua masuala na pia kutoyumbayumba, na ambayo ilikuwa na utajiri wa matokeo kwenye mijadala, hadi kufikia kulipandisha hadhi tamasha hilo likawa ni la kutoa manufaa makubwa zaidi ya yote yaliyowahi kutokea awali.’

# UZINDUZI NA TAMASHA ZA JUKWA LA FEMINIST REPUBLIK - KUENDELEA...

Jukwa la Feminist Republik liliweza kuanzishwa kutokana na mahitaji ya watetezi wa haki za kibinadamu za wanawake wa Afrika ya kuwa na suluhisho zenye asili katika bara hili, na ambazo zingeongezea mseto wa mbinu nyingi zenye ubunifu wa kuchokoza, kuchecheta na kuwahimiza watetezi wa barani kuweza kuwaza upya na kuchochea mabadiliko ya mitazamo ili kuwezesha kuelekeza juhudi za kupata bara ambalo litakuwa huru bila machungu na mahangaiko. Baraza hili lilitambua na kuenzi kuwepo kwa utajiri wa busara kwenye nafasi inayozingira masuala ya uponyaji. Ilikuwa ni hatua ya ujasiri mkubwa sana ambayo iliwawezesha washiriki 315 kushuhudia uwanja ambao ulidhihirisha wingi wa mawezekano yasiyo na kikomo ambayo yanaweza kutumiwa na wahusika binafsi au hata kwenye swala zima la uponyaji wa pamoja.

Ilikuwa ni ajabu sana jinsi ambavyo tamasha hili la siku 3 liliweza kutilia mkazo juhudi nyingi za wafeministi mbalimbali na hata pia kuboresha ujuzi wao, busara  na maarifa kuhusu uponyaji na utunzaji kama njia ambazo zinaweza kutumika kutuimarisha na kutuongezea ari zaidi kama watu binafsi na hata harakati zetu kuendelea kunawiri. Iilikuwa jambo la kutia moyo kuona jinsi ambavyo siku hizo 3 ziliweza kutumika kuhalalisha mbinu nyingi za uponyaji na utunzaji. Iilikuwa na umuhimu wa kuhalalisha mbinu za uponyaji na utunzaji ambazo zilitumika kiasili katika bara la Afrika, na jinsi ambavyo mbinu hizi zinaambatana na zile za kisasa za kuweza kutia katika kujitunza na kujijali sisi wenyewe binafsi. Kupitia kwa mkutano wa jumla ya wahusika wote, na pia kwa vikao maalum vilivyoendelea kwa wakati mmoja, wahusika waliweza kushuhudia nguvu zilizobubujika, fadhili, katika nafasi iliyowapa washiriki fursa ya kushiriki uzoefu, kujadiliana, kuhimizana na kuongezana nguvu, ukarimu...ni haya ndiyo yaliyopelekea wakati huo na nafasi hiyo kuwa spesheli.

Hi tamasha ilikuwa nafasi muhimu ya kubadilisha maisha kwa kila awaye yule binafsi na pamoja kwa wote waliohudhuria.

Mijadala iliyoandaliwa ilihusu masuala mbalimbali na mitazamo au mbinu za kuweza kuwaza kwa upana na kutoa msingi wa ujumla wa usalama, ustawi na ukuzaji wa maarifa kwa wafeministi na harakati za humu barani Afrika. Walikwa mashuhuri waliohutubia vikao walieleza washiriki misingi ya kisiasa ya kuunga mkono umuhimu wa kujitunza kibinafsi na utunzaji wa pamoja, na ya kwamba ni kwa nini silo jambo la kusubiri tena. Mijadala pia ilihusu umuhimu wa mshikamano, huku wengi baadhi ya waliohutubu wakitumia fursa yao kwenye jukwaa kushiriki, kusikiliza na kujiunga kwa kuchangia mijadala ya pamoja kuhusu ni nini kinachohitajika ili kujibadilisha wenyewe binafsi na jamii zetu ili kuelekea na kukumbatia utamaduni wa uponyaji na ustawi.

# UZINDUZI WA FEMINIST REPUBLIK

Kule tu kuwa miongoni mwa wengi ambao, hata kunako uhasama, walijitolea kushiriki hadithi zao za kuhimiza ila ambazo wakati mwingine zilikuwa ni za ujasiri, nguvu na kujiamini. Mavuno kwenye tamasha hii yalikuwa ni kujaribu kuwa na uzoefu wa ulimwengu wa uponyaji, utunzaji wa mwenyewe binafsi na wa jamii, na kuyachanganua mawazo haya na vitendo katika aina zote ziwezekanavyo.

Katika nafasi hii, kulikuwa na wakati wa kutosha kwa wanawake kuchukua muda kuweza kuunganishwa tena na wandani wa zamani na wageni, kushiriki tabasamu, kuungana na nafsi zao wenyewe, kupata wasia wa kutia moyo na ufungamano. Ratiba iliundwa ili iwe ya kusudi, kutoa muda kwa ukarimu ili washiriki waweze kukatiza kwa mapumziko, na kwa kujitunza wenyewe binafsi na kuwatunza wenzao. Harakati za wafeministi wa Afrika zinahitaji njia bunifu na zinazo wajali wanaharakati ili kukumbana na changamoto na mapambano ambayo ni ya kipekee. Wasanii wanatumia sanaa zao kuvuruga maeneo yaliyopo na ya kidijitali. Wanaotafakari kwa ubunifu wanalazimisha hotuba mbadala ambazo zinavuruga mawazo ya kawaida kuhusu miili, jinsia na ujinsia.

**"Iilitoa fursa kwa kila mmoja kibinafsi au kwa pamoja kufikiria na kujaribu kujibu hili swali, "Je! Tunaweza kufanya nini kuleta uponyaji na kinga Afrika, kwetu sisi wenyewe, kwa jamii zetu? Njia ambayo ni zaidi ya kiwewe chetu na mahali au nafasi ya kujipata katika upendo na huruma?"**

Chakula cha jioni na uzinduzi huo kilikuwa matukio yasiyosahaulika kwa sababu ilitoa nafasi ya kusherehekea, kutoa heshima kwa ukakamavu wa watetezi wa haki za binadamu wa Kiafrika, wa tangu zamani na wa sasa. Pia ilitoa fursa ya kuanzishwa kwa enzi mpya, ufufuaji wa utamaduni ambapo tunaweka utunzaji usio wa kawaida wa kibinafsi na wa pamoja moyoni mwa kuwa ni jinsi gani na ni wapi wanawake, wanaharakati na harakati zinafanya kazi.

Huo uzinduzi ulikuwa ishara ya ufikiaji wa mipaka mipya ambapo kila mmojawapo wa washiriki wangerudi makwao na kujuinga upya na kila mmoja wa wenzao kujadili njia mpya za kuwepo, za kuendesha harakati na hata kudunisha vile vizuizi ambavyo kwa muda sasa vimesababisha miili yetu, roho zetu, harakati zetu na utetezi wetu kukwama kwenye dhiki. Hebu furahia mtandazo wa picha ambazo zinadhihirisha safu ya mihemko, mazoezi ya uwazo, tafakari na misaada iliyoshirikiwa kwenye kongamano. Tukiwa tumeiacha nyuma yetu uzinduzi na tamasha hiyo, daraja la kujifunza na kutekeleza uponyaji wetu linajengwa sasa...Na hakuna kurudi nyuma Kamwe!

Safari ya hatua 1,000 huanza na hatua moja kwa kila wakati....

Mapambano bado yataendelea......

Aluta Continua...

# JITUMBUIZE NA PICHA KUTOKA TAMASHA NA UZINDUZI WA FEMINIST REPUBLIK!












# PICHA KUTOKA TAMASHA NA UZINDUZI WA FEMINIST REPUBLIK!











# PICHA KUTOKA TAMASHA NA UZINDUZI WA FEMINIST REPUBLIK!









# PICHA KUTOKA TAMASHA NA UZINDUZI WA FEMINIST REPUBLIK!












# PICHA KUTOKA TAMASHA NA UZINDUZI WA FEMINIST REPUBLIK!








# PICHA KUTOKA TAMASHA NA UZINDUZI WA FEMINIST REPUBLIK!















# Jukwa la Feminist Republik limewasili, na linaendelea kubadilika kuwa bora

**Masa Amir**

Pamoja na uelewa wa Hazina hii wa muktadha ambamo kazi inafanyika, msaada uliopo na mapengo yanayohitajika kushughulikiwa, shirika la UAF-Africa liliweza kuandaa kongamano la wahusika 45 la WHRD kutoka barani Afrika jijini Abuja, Nigeria kuanzia tarehe 13 hadi 15 Julai 2018 ili kuwezesha mkutano wa mtiririko wa mawazo na mashauriano ambapo pia shirika lilitaka kuhalalisha pendekezo la awali la kwamba jukwaa kama vile lile la Feminist Republik linahitajika. Bila shaka kulikuwa na maafikiano ya kwamba jukwaa kama hili lina umuhimu, na mawazo mengi yaliweza kuchipuza kuhusu majukumu mbalimbali yanayoweza kutekelezwa na jukwaa kama hilo; aina ya mada za kupewa vipaumbele; njia za kuhusika, mfumo wa jukwaa lenyewe, wadau wa kuhusishwa kwenye jukwaa hilo, lugha mbalimbali za kanda ambazo zinaweza kutumika; ubia au ushirika ambao unaweza kuundwa, miongoni mwa majadiliano mengine mengi ya kusisimua, na ambayo yaliashiria mchanganyiko wa changamoto ambazo WHRD, kutoka pembe zote za bara hili wanakumbana nazo. Mkutano huo wa Abuja ulianza kulibingirisha gurudumu la kuweza kuanzisha jukwa kamilifu na la kijumla la ulinzi, usalama, ustawi na utunzaji wa pamoja wa Watetezi wa Haki za Kibinadamu za Wanawake wa bara la Afrika, jukwaa ambalo watetezi wataunda kwa pamoja nafasi bunifu ambayo ni muhimu kwa marejesho ya roho, uponyaji na ustawi kwa wao weyewe.

Wazo katika shirika la UAF-Africa la kuanzishwa kwa jukwaa ambalo linalenga kuwa nguzo kwa Watetezi wa Haki za Kibinadamu za Wanawake almaarufu Women's Human Rights Defenders (WHRD) katika bara la Afrika ni wazo ambalo limekuwa likipikika kwa miaka kadhaa sasa. Kote ulimwenguni, wana WHRD wamekuwa wakifanya kazi yao katika mazingira mbalimbali ya kisiasa ya vurugu na ugandamizaji, kuchunguzwa, ukosefu wa usalama, kuvamiwa na hata kutishwa.

Kwa miaka mitano iliyopita, ikiwa inaambatana na hali ya ulimwenguni kote ya kuanza na kuzowea kuyatumia matamshi "kubanwa kwa nafasi za mashirika ya kiraia', shirika la UAF-Africa limekuwa likifuatilia kwa karibu ongezeko la mienendo fulani ya kusikitisha, kukusanya taarifa kutoka vyanzo mbalimbali kuhusu miktadha ambamo WHRD wa barani Afrika wanafanyia kazi zao.

Hii ni pamoja na taarifa za kiuchunguzi ambazo tumeweza kuzikusanya kutokana na huduma zetu za kutoa ruzuku za dharura (ikiwa ni pamoja na ongezeko thabiti la ruzuku za ulinzi kutoka asilimia 28% ya ruzuku zote zilizotolewa na shirika mnamo 2012 hadi takriban asilimia 40 mnamo 2017 na 46% katika mwaka wa 2019); tafakari na uzoefu ambao wana WHRD walishiriki kwenye mikutano na matukio chini ya miradi yetu ya Utetezi na Kujenga Miungano, almaarufu Advocacy & Alliance Building programme, (na hususan mkutano wa kimataifa kuhusu kuendelea kubanwa kwa nafasi za mashirika ya kijamii ambao uliandaliwa nchini Kenya na shirika la UAF-Afrika mnamo Julai 2017, na ambao uliwezeshwa kwa mchango wenye ukarimu mkubwa kutoka kwa program ya Haki za Wanawake ya shirika la OSF.), na lile tokeo la mkutano huo ambayo ilikuwa ni ripoti ya ulimwengu ambayo iliwezeshwa na udhamini kutoka mahirimu almaarufu UAF Sister Funds kuhusu dhihirisho mbalimbali za kubanwa kwa nafasi ya shughuli za mashirika ya kiraia na kuangazia uzoefu wa utetezi wa wahusika wa WHRD katika maeneo yote ambamo hao madada wanafanyia kazi za utetezi.

Inanuiwa na kudhamiriwa ya kwamba mpangilio huu wa Feminist Republik itakuwa ni nafasi muhimu ya kujitulizia wenyewe kutokana na uchovu na dhiki, kutu, mmomonyoko wa moyo, akili na mwili ambao hutokana na utetezi; kutoa msaada kwa wenzao na kujichangamsha upya.

*"Sisi ni watu wenye kuota ndoto kubwa sana, na bila shaka tuna njozi kubwa kuhusu jukwa hili la Feminist Republik - kuanzisha shamba la uponyaji ambalo litakuwa ni nafasi muhimu ya mapumziko, kujiunganisha tena na asili, mahala pa watetezi wa WHRD kukutana na kuungana, au hata kwa madhumuni mengine ambayo yataamuliwa na watetezi wa WHRD....'*

Kulikuwa na maafikiano ya kwamba nafasi hii itatumika kuwaleta pamoja watetezi wa kifeministi, wale wenye uwezo wa kuwa wahusika na washirika kufanya kazi kwa njia ambazo zinaimarisha na kutoa kipaumbele kwa mahitaji, dhamira, matumaini na ndoto za watetezi barani Afrika na kuweka bidii kuelekea kuimarishwa kwa haki za watetezi huku wakikuza uwepo upatikanaji wa haki ya kisheria kupitia uwekaji wa kumbukumbu na kupambana na ukatili na ukiukaji ambao watetezi wa haki za wanawake wanakumbana nao katika nafasi mbalimbali wanamofanyia shughuli zao. Jukwa hili la Feminist Republik litalenga kuhakikisha hususan vyombo vitatu vya kazi: Ukamilifu (kinga) ulinzi, usalama, ustawi na utunzaji wa pamoja; Uponyaji kupitia Haki ya Kisheria; na Uwekaji wa Kumbukumbu na Kuzalisha Maarifa.
Tulifanya mkutano wetu wa mwisho wa mashauriano na wadau mbali mbali mnamo Februari 2020 ku toa taarifa juu ya mipango yetu na unaweza kusoma juu yake katika ripoti yetu juu ya kiunga hiki.
Tunayo ndoto pia ya kuunda eneo la usajili katika ukanda ili kufuatilia aina za dhuluma na wingi wa matukio au marudio ya dhuluma hizo dhidi ya WHRD katika bara hili; na kushughulikia utafiti wa kipekee kuhusu uponyaji wa haki ya kisheria kama mtazamo unaoweza kutumika na harakati za kifeministi ili kupambana na viwewe vya kihistoria na zilizopokezwa vizazi, na kubuni nafasi za uponyaji.
Nyingi baadhi ya michakato hii tayari imeanza na tuna mipango ya kushiriki sasisho tunavyoendelea! Tuna furaha kubwa iliyoje tunapoianza hii safari kuu tukiandamana na washirika wa kifeministi, washauri, watendaji wataalam na watetezi ambao wanaandamana nasi na kutupatia mwongozo katika mchakato huu. Tuna furaha kubwa hata zaidi ya kwamba majadiliano, mashauriano na michakato ya tafakari za pamoja ambayo tumeweza kuhusika nayo mnamo miaka hii miwili iliyopita imeweza kutuleta hadi katika sehemu hii kwenye safari hii ya kusisimua ya kutekeleza ukweli wa kujenga jukwaa na nafasi ambazo zitachangia kwa uangalifu siku za usoni za kifeministi.



# TUNAKUA TUNAVYOJALIWA

## JINSIA NA GONJWA LA COVID-19

NA SOLOME NAKAWEESI AND MELISSA WAINAINA

Pwaaaa.. Pwaaa.. Pwaaaa.. Inafika saa sita usiku; baruti zililipuka, zikiangaza angani! Boom.. boom ... boom, mirindimo ya ngoma iliongezeka ndani ya vijiji mbali mbali vya Kiafrika huku kuimba, kukumbatiana na kucheza kumalizia wakati huo wa shangwe kuu. Vijijini au mijini, matajiri au masikini, vijana au wazee, wanaojiweza au walemavu, tulikaribisha 2020, kutupeleka ndani sio mwaka mpya tu lakini muongo mpya! Matumaini, matarajio, uwezekano, wasiwasi, ndoto ambazo sisi wote tulipata mnamo mwaka wa 2020.

Kama harakati na wanaharakati wa kifeministi barani Afrika, tuliingia mwaka 2020 pamoja na utata wetu na mashindano katika kukuza usawa wa kijinsia na haki za wanawake na bado kukiwa na mapungufu ya usawa. Harakati za kifeministi katika Afrika na kwingineko zimeonyesha utulivu na uvumilivu zaidi ya miaka ili kudai tena nguvu ya kuvuruga hali ilivyo na kubadilisha mwenendo wa dhulma za kihistoria. Hakika, tulikuwa tumeona aina nyingi za ushindi na pia kushindwa kwingi.. Tumefurahi kwa shangwe na kwa usawa kama vile tulilia na kufadhaika.. Tulikuwa na ndoto kubwa kwa 2020.

Mwaka Mpya ulileta 'upya' fulani kwa vita ambavyo vinavyojulikana vya haki na mabadiliko ya kudumu. Hiyo inasemwa, maisha kama tunavyojua hutoa mkusanyiko wa mabadiliko mengi ya kustaajabisha, na mengine huja kwa njia za kushangaza ambazo zinahitaji umakini wetu kamili. Janga la kidunia la COVID-19 ni moja wapo ya mifano hii. Gonjwa hili limezorotesha hali ambazo zilikuwa zinatukumba tayari za kutokuepo usawa na udhaifu uliopo tayari kwa masuala ya jinsia, rangi, kabila, tabaka na migawanyiko mingine ya kijamii. Hivi sasa tunakabiliwa na mgogoro ambao una pembe nyingi - afya, utunzaji na shida ya kiuchumi ya viwango vya ulimwengu. Kuibuka kwa ukosefu wa usawa uliokaa ndani kwa muda una athari nyingi kwa afya na ustawi, kujikimu kimaisha yetu na utulivu.

# JINSIA
# NA GONJWA LA COVID-19

*"Wanawake na jamii zingine zilizopuuzwa zina mzigo mkubwa wa ukosefu wa kinga ya kijamii na mifumo na taasisi zilizoshindwa na ambazo hutoa vipaumbele kwa utunzaji na ustawi wa jamii zake."*

Uchumi umezorota kabisa, familia hazina chakula, ili hali dunia inapita katika janga la ulimwengu ambalo linatishia ustaarabu wa kisasa na pia kutoa fursa ya uwezekano wa "Mfumo mpya na wa kusisimua zaidi wa ulimwengu."

Kama Harakati za Kiafrika, lazima tupate suluhisho za Kiafrika ambazo zinajibu utofauti wa jinsi janga hili lidhihirika barani Afrika na watu mbali mbali. Kwa mfano, moja ya vifaa muhimu zaidi kudhibiti kuzuka ni kupitia afya ya umma. Ukweli hata hivyo ni kwamba kuna mapungufu makubwa katika mifumo mingi ya afya ya umma barani Afrika ili kujibu na kuchukua hatua za kupunguza kuenea kwa janga hili. Mitindo ya ubepari ambayo ndiyo imetanda ilishindwa kuwalinda watu wake wakabaki hatarini na wasio tayari au na uwezo waa kustahimili COVID-19 na kusababisha shida zaidi. Kila siku tunaona huduma dhaifu za kiafya, wafanyikazi wa huduma ya afya wenye mishahara duni wanaweza kuashiria ushawishi wa aina ya uchumi unaotegemea huria mamboleo ambao sasa unachukuliwa kuwa hauwezi kukabiliana na janga hili kwa njia ambazo zinazingatia mahitaji ya watu na utunzaji. Ukweli kwamba vifo vya akina mama, ubakaji, uchumbaji wa wahusika, utoaji mimba usio salama na dhuluma inayotokana na jinsia imeenea wakati wa kufungwa kwa bara hili ni kiashiria dhahiri kwamba mabadiliko makubwa lazima yafanyike mara moja.

Kutokuwa na usawa wa kijinsia ni suala la wafeministi. Dhamira muhimu ya hii ni kushughulikia sababu za kimsingi za ukosefu wa usawa wa kijinsia na wa kimfumo na kuchanganua hali ya mahusiano ya kijinsia na kutokuwepo usawa wa nguvu uliopo katika makundi haya. Ni muhimu pia kuchambua njia ambazo aina tofauti za ubaguzi na kutengwa zinafanya kazi pamoja. Wanawake huajiria katika zaidi ya kazi za utunzaji, ziwe za kulipwa na zisizo za kulipwa ulimwenguni kote na sio tofauti barani Afrika. Gonjwa la COVID-19 linasababisha uchumi dhaifu wa utunzaji kuzorota hata zaidi. Yanayodhihirika zaidi ni hali duni za kufanya kazi bila kinga ya kijamii na kiajira. Uchumi wa utunzaji haujawahi kupata tahadhari ya kweli katika sera kushughulikia sababu za kimuundo za ukosefu wa usawa wa kijinsia katika uchumi.




"Afrika katika yote haya imethibitisha hali ya uvumilivu na uvumbuzi ambayo ulimwengu kwa mara nyingi unayapuuza - na wanaoiimarisha hali hii ya kupanda na kuongezeka ni wale ambao hawajatambuliwa kikamilifu, wanawake wake.."

# JINSIA
# NA GONJWA LA COVID-19

Hili linaposemwa, bara hili ni muhimu lijitayarishe kukabiliana na shida nyingi sana ikiwa pamoja na kupambana na ubeberu ambao ingawa wakoloni walienda, athari zake bado zimekithiri miongoni mwa taasisi na katika uchumi. Bara la Afrika lilitambua haja ya kuwekeza katika mfumo wake mwenyewe wa afya na kwa wakati huo; kukubaliana kwamba mfumo wa mwitikio wa COVID – 19 ulichangia kuongezeka kutokuwepo kwa usawa kupitia: kuvurugika kwa tabia za kawaida za jamii (kama vile kutotangamana kwa karibu), ongezeko la visa vya ukatili wa kingono na kijinsia (kwa vile wanawake na wasichana wanazuiliwa na kufungiwa na wahusika ndani ya nyumba hizo).

Afrika imeishi kupitia sio utumwa wa watu wake tu, na pia kupokonywa maeneo walioita makwao lakini pia majaribio ya kuharibu makabila yetu, tamaduni zetu na ufahamu wetu. Afrika iliishi kupitia hatua za ukali wa madhubuti ya matumizi ya fedha katika miaka ya 70 na 80 ambapo pia kulishuhudiwa mabadiliko kwa nguvu kutoka kwa serikali kwenda kwa mifumo ya huria mamboleo ambayo iliona sekta zetu muhimu za umma ambazo zinatoa usalama wa kijamii kwa raia wa kawaida (huduma ya afya, elimu, miundombinu) kubinafsishwa.

Kwa njia nyingi hii ndio sababu tunaona wanawake kwenye safu za mbele za uchumi wa huduma za afya na uchumi wa utunzaji na kubeba sehemu kubwa ya kazi ili kudumisha ustawi wa jamii zao. Na asilimia 70 ya wafanyikazi wa kiafrika barani Afrika ni wanawake wanaopata fidia kidogo au hawapewi fidia mara nyingi kutoa hela ndani ya mifuko yao kutekeleza majukumu yao ya utunzaji (Umoja wa Mataifa, 2019). Kwa kuongezea, na mifumo ya majibu ya COVID-19 kama 'kaa nyumbani', 'uthibiti wa shuguli' na 'kutotangamana kwa jamii' ilichangia wanawake wengi wakiongezeka kwenye kazi ya utunzaji bila kulipwa, ukosefu wa ajira na wanakabiliwa na ukiukwaji mkubwa (kimwili, kihemko, kimapenzi na kifedha). Kwa kuongezea, sera za kutotangamana kijamii zimefuruga kukusanyika na kufanya kazi kwa wanawake wa Kiafrika na nafasi salama ambazo zilikuwa kihistoria kupitia vikundi mbali mbali vya uchumi wa kijamii, nafasi salama, mkusanyiko na mashirika. Usisitizo wa utumiaji wa nafasi za mtandaoni kufanya kazi na kukusanyika huongeza gharama ya kushirikiana, hautilii maanani maswala ya usawa wa wanawake na watu masikini katika ukifikiaji wa teknojia na; nafasi za kidijitali ambazo hazijatengwa kutilia maanani huo mgawanyiko wa kiuchumi wa kijamii, kuongezea umaskini kwa wakati wa wanawake ulemavu na uhamasishaji wa ufeministi.

Afrika imeishikupitia wakati huu wote; janga hili ni fursa ya kuleta mambo mengi - mengine magumu sana kukabili kuliko mengine. Fursa ambayo inatokea ikiwa ni sisi kufikiria upya vipaumbele vyetu. Janga hilo linatoa Afrika kwa urithi wake ambao ni utajiri wa kitamaduni, mifumo ya kusaidiana katika jamii, vitendo vya ustawi na baadhi ya mimea ambayo imekuwa ikitumika kuendeleza jamii wakati wa janga. Kusonga mbele, tunapojenga harakati endelevu barani Afrika, inabidi tusimamishe shuguli, tuchukue nafasi ya kurudi nyuma, tujisikilize wenyewe binafsi na kwa umoja wetu, na kubuni kwa pamoja kwa njia za uponyaji na huhakikisha kwamba tumeziteleza njia hizi kwa kazi zetu.

Muhimu zaidi, ni sisi kushiriki kuendelea kugundua njia hizi za utunzaji na uponyaji - kwa sababu COVID-19 ni virusi ambavyo viko hapa nasi na kustawi wakati wa janga hili ni mojawapo ya aina za ukakamavu. Kama wanawake wa Kiafrika, kulichanguna janga hili tukitumia mtazamo wa kijinsia kunahitaji tuweze kuimarisha nyayo zetu, kugeuza na kuelezea hadithi zetu za ujasiri na jinsi tulivyokabiliana na janga hili lisilo la kawaida la ulimwengu kushiriki hadithi za jinsi kawaida tunavyostahimili na kustawi - lazima tuhakikishe mfumodume, ubaguzi wa rangi, ubeberu, ukoloni mamboleo, kutokubali ujinsia mbadala na ya aina zote za ukandamizaji zimeondolewa kwetu kama watetezi wa haki za binadamu wa Kiafrika. Lazima tuidai nafasi hii ya kidijitali na kuifanya iweze kutajirika na kutumika kikamilifu badala ya kuchoka na kutumaliza nguvu, lazima tuliongeze hili kwenye 'Uafrika' wetu wa kushiriki hadithi tukiota moto usiku. Ndio, hapa ni mahali pa kuota moto huku tukishiriki jinsi tuko na uvumilivu, ustahimilivu, utahatarishi lakini pia wenye nguvu.

Tunamalizia kwa kukupa changamoto: Je! Ni nini “Mpya ya kawaida’ na hii itaiga mifano ya ukosefu wa usawa wa kijinsia iliyopo au itaruhusu kuvunja minyororo ya utumwa au tu kuimarisha na kuthibitisha kutokuweko usawa kwa wanawake na ukandamizaji? Je! Itavunjamzigo unaowekwa na ubaguzi kwa Waafrika, watu weusi na watu wa rangi au zaidi? Je! Itakubali .. Tunakuachia haya uyatafakari kwa kina.

Kuna haja ya kujikomboa….



# MKUSANYIKO WA MITANDAONI WA UBUNTU NA 'MOON GODDESS'

NA ZANELE MBUGUA

**"Ulimwengu una njia zake ambazo hatimaye hufunga vitu vizuri na kuunda tovuti yenye tandu ngumu iliyoimarika!"**

Ingawa jukwaa la Feminist Republik lilianzishwa karibu kufikia mwisho wa mwaka wa 2019, shughuli zake rasmi zilianza mnamo 2020 wakati hatari za janga la Corona zilianza kuenea kama moto mbaya sana - na kwa mchakato huu likaunda woga, wasiwasi, kutokuwa na uhakika, kuhusu idadi ya vifo, maambukizi kuongezeka, hali ya kutokuwa na la kufanya na mabadiliko makubwa ya maisha yetu.

Jukwaa la Feminist Republik katika kusaidia kutatua hili, lilifikiria jinsi ya kushiriki katika kupunguza matatizo ya kiuwili, kijamii na kisaikolojia ambayo wanaharakati na wafeministi walikuwa wanakabiliwa nayo. Baada ya mashauriano mapana, ilikuwa wazi kwamba nafasi halisi na mkutano ulikuwa muhimu kusaidia, kushikilia na kupunguza mzigo kwa marafiki wapya na wale wa zamani au washiriki wa jukwaa la Feminist Republik. Mkusanyiko wa mitandaoni wa Ubuntu ulizaliwa!

Mwenyeji wetu kwa mkusanyiko wa mkutano huo alikuwa rafiki wa zamani wa jukwaa hilo, Dk Toyin Ajao maarufu kama ' Moon Goddess'. Tulipojadili kwa kina masuala kuhusu mkusanyiko huo kwa kushirikiana na naye, alitoa maoni ambayo yalikuwa pia ni hisia ya wengi miongoni mwa washirika kwamba tangu janga hili liligonga, watu walikuwa wanakabiliwa na vitu vingi ambavyo hutokana na kutokuwa na uhakika, wasiwasi na hofu inayohusishwa na virusi hivi.

Kulikuwa na haja ya kuundwa kwa nafasi ya mtu kuja tu kama alivyo, kulikuwa na hitaji la nafasi ambayo wasiwasi wetu wote kwa pamoja na udhaifu utakubaliwa upo lakini pia kuunda msingi dhabiti wa pamoja wa wakala huu. Na kisha... safari ya Mkusanyiko wa Ubuntu ilianza.... Nafasi maalum ilitengenezwa ili kuwezesha wanaharakati watetezi wa haki ambao ni wanawake, wabadili jinsia, na wasiojiambatanisha na jinsia yoyote kufurahia, kupiga kelele, kulia, kucheza; kujivinjari na glasi yako ya mvinyo nyumbani wakiwa na uwezo wa kupatanishwa kidijitali na wenzao barani Afrika na hata kwingineko ulimwenguni.

**Kila Ijumaa, tulikuwa wenyeji wa Jukwaa la Mkusanyiko wa Ubuntu ambalolilikuwa na jukumu la kisiasa la kutoa ukumbusho wenye ukweli ila kwa njia ya upole kwamba ilikuwa ni muhimu kwa washiriki wetu kutoa kipaumbele kwa maslahi yao binafsi na pia muungano wao kama wanawake watetezi wa haki za kibinadamu wa Kiafrika.**

Hadi leo, jukwaa la Feminist Republik limeandaa mikusanyiko sita ya kila wiki, ambapo Moon Goddess aliwasilisha vizuri kwa mada na matendo anuwai. Kutoka kwa kucheza ngoma ya Yemoja Dance na Happy Hour Café hadi wimbo wa Kujijua Song na Skana ya kujijua mwili kwa ujumla, maandishi ya kujieleza ya Gursha, mviringo wa uponyaji wa Ubuntu Healing Circle na hata Glow Yoga, yote haya yakijumuisha utafiti wake wa vitendo, kushirikiana kwake na uzoefu wake katika uponyaji wa mabadiliko. Yote ambayo wageni walihitaji kufanya ilikuwa kufika mahala pale na kuamua wenyewe jinsi ya kuchunguza kwa makini nafasi ile; kitu chochote kutoka kwa uchunguzi wa kimya hadi mwingiliano makini. Machozi yalimwagika, mambo mapya yalifunzwa, nyimbo ziliwafurahisha, urafiki mpya ulianzishwa na tulijizatiti kuendelea na mkusanyiko licha ya mitafaruku hapa na pale ya kiufundi na kuunganishwa tena mara kwa mara kwa mitambo.

Jukwaa la Feminist Republik linafanya kazi kwa kushirikiana mara kwa mara na washirika na marafiki, na hivi karibuni hashtagi #FRFridays iliundwa ambapo mtu anaweza kufuatilia mikusanyiko yetu yote na shughuli za mitandao ya kijamii. Huo ulikuwa ni mkutano wetu wa kwanza uliomualika yeyote yule baada ya uzinduzi wetu na tafrija iliyofanyika mnamo Desemba mwaka wa 2019. Tunafurahi kubaki kambi na nanga katika kusaidia wanawake watetezi wa haki za binadamu wa Kiafrika ili wajijenge na harakati zao kama watu wenye nguvu na wenye kujikakamua zaidi kupitia misiba na mengine mengi.

Moon Goddess anaeleza ya kwamba matokeo yasiyotarajiwa na ule ujumla wa Mkusanyiko wa Ubuntu ni mambo yaliyohitajika kwani ni mkutano huo uliundwa kwa kuwanufaisha wale watu wanaoitumia:

“

**"Unaweza kufanya kazi tu iwapo wewe mwenyewe umejazwa. Ikiwa nguvu zako zimepungua, utawezaje wewe mwenyewe binafsi kusukumiza hata yale mabadiliko unayotaka kuona ulimwenguni? Na ikiwa tutaendelea kujipuuza, ili tu tuendelee kupigania usawa, tutajikuta tunakosa nguvu ya kupambana tena na tena. "**

**Moon Goddess**

Kwa upande wa washiriki wa Mkusanyiko wa Ubuntu, wengine walielezea kwamba kurudi kwao kwenye mkusanyiko mara kwa mara ilikuwa ni kwa sababu anuwai ya utofauti wa hoja walizoshiriki kwa pamoja katika kila kikao, lakini pia bidii na mori ya Moon Goddess, fikira, upendo na hisani ambao ulitolewa na kushirikiwa katika nafasi hizi. Washiriki walijiona wakiwa pasi peke yao katika uzoefu wao na uhatarishi hata kwa wale ambao wakati wote walikuwa wamekaa kimya katika nafasi hiyo. Kwa wengine, mkutano huo ulikuwa ukumbusho wa juma refu. Na kwa wengine, walikuwa wakitamani kusikia habari zake tu kwa hivyo waliendelea kurudi kwa zaidi....

Hakikisha usikose kuhudhuria mkusanyiko wetu utakaoufuata wa kidijitali wa jukwaa la Feminist Republik!

# Kukusanya Washiriki wa Ubuntu

KUUNGANA
KATIKA WAKATI WA MGOGOROBUNTU

SAUTI YA WASHIRIKI WETU

Na Shinaz Ali and Zanele Mbugua

**Jukwaa la kukusanyika la Ubuntu lilipata wafuasi waaminifu miongoni mwa marafiki wa Feminist Republik. Baada ya kusikia kuhusu mkutano huo, baadhi ya washiriki walikiri kwamba walijiunga kudadisi tu, wengine walivutiwa na jina la jukwaa hilo au mada ya kikao, ila wengine walishangazwa na jina tu. Wakati ambapo baaadhi walijiunga ili wawe katika jamii ya vitendo kuhusu utunzaji uponyaji, kupata nasafi salama ya kufungua roho na kupakia kuweza kujiendelesha katika hali ya kukosa uhakika maishani.**

**Kuongezea kwa vitendo vyao vya ustawi, kushiriki na wengine na hali kadhalika, kunawiri na kupitia kwenye uwoga, wasiwasi, habari hasi za mara kwa mara, kuhusu vifoo na maambukizi.
Kusitishwa kiasi au kikamilifu kwa shuguli za kila siku. Unyanyasaji wa kingono na kijinsia, njaa, ukosefu wa makao na hali ya kutokuwa na uwezo kuyatatua matatitzo na hiyo mifumo yote ya kupambanana na janga la COVID19 ambayo watu wengi Afrika na kote duniani wana kumbabana nayo. Baada ya kuwa na uzowefu wa mikusanyiko ya Ubuntu, washiriki walisema kwamba walifurahia sana ari na ujamii ya vikao vyao.....Wengi waliendelea kurudi wiki baada ya nyingine.**

**Timu ya Feminist Republik iliwatafuta na kuwahoji watu wa miongoni wa washiriki hao baada ya msururu huo wa wiki sita kudadisi kwa kina uzoefu wa binafsi na maoni yao kuhusu Mkusanyiko huo.**



**Cynthia Happi (CH) - ni raia wa Kamerun ambaye kwa sasa anaishi na kufanya kazi nchini Ethiopia kama Mtafiti wa Amani na Ulinzi. Cynthia ni mpenda muziki ambaye pia ana shauku ya soka.**



**eloise burke (eb) - ni mtaalam wa maendeleo ambaye asili yake kama mtu wa Kiafrika aliye bila makazi na wa Kiafrika-Karibian na nchi ya Kanada, na umempa uzoefu mbalimbali, uwekezaji, ujanja uliojaa mmarifa, na ujuzi wa hali ya juu ambao ni wa kipekee kwa njia yangu.**



**FFrançoise Moudouthe (FM) - ni Mfeministi wa Muungano wa Afrika na mwanzilishi wa Eyala, jukwaa la lugha mbili ambalo linatumia Ushawishi wa mazungumzo ili kuchunguza kwa kina maana ya kuwa mfeministi katika bara la Afrika wakati huu.**

**Ni nini ulifurahia zaidi katika ile Mikutano ya Ubuntu?**

eb:Kuwa katika nafasi hiyo na hisia za undugu hufanya mtu asisimke. Nilipata vikiwa vikao vya kutia moyo sana sana. Hasa kwa wakati huu ambapo sisi, kibinafsi kadiri inavyonihusu, tunakuwa chini ya sheria ya kusitishwa shughuli zote. Lakini haswa Moon Goddess ni mwangaza maalum sana, na sina uhakika kama mtu mwingine angekuwa na athari sawa na yake kwangu mimi, kama alivyofanya kwa njia ya jinsi alivyotuelekeza kupitia vikao, kuwa nasi kwa njia ambayo alifanya. Nafasi hiyo ilinipa fursa ya kukua kwa uelewa na ni kana kwamba vikao vilikuwa vimepangwa na ulimwengu maalum kwangu. Kwa hivyo, kwa maana hiyo, vilikuwa maalum kwangu na vile vile hali ya mimi kuwa mbele ya viumbe wengine ambao kwamba licha ya uzoefu wao, sote tulikuwa tukijiburudisha sawasawa. Na kwangu mimi kucheza densi ni muhimu sana.

**Mbona ulijiunga na mkutano wa kwanza wa Ubuntu? Uliona kwamba utanufaika na nini?**

CH: Katika moja ya mikutano hiyo ya mitandaoni, nilishiriki wimbo ambao ulikuwa kama muhtasari wa changamoto zangu, hofu na safari yangu ya maisha. Nilipokea msaada mkubwa sana kutoka kwa mkutano huo wakati ulipokuwa unaendelea na hii ilikuwa hatua ya kugeuza safari yangu ya uponyaji. Niliweza kuhisi msaada kutoka kwa wengine. Nilihisi watu wakijaribu kuwa kwenye nafsi yangu na waliweza kunitumia nguvu zao zote nzuri.

**Mimi najua ya kwamba wewe ni mmoja wa watu ambao wamehudhuria Mikutano ya Ubuntu kila Ijumaa bila kukosa, mbona ulihakikisha kuhudhuria kila kikao?**

FM: Kwanza, nafasi yoyote na Wafeministi wa Kiafrika ni mahali pa furaha yangu! Mimi ni bingwa mkubwa wa nafasi ambazo Wafeministi wa Kiafrika wanaweza kukusanyika na kuwa wahai wao kamili, walio katika hali ya hatari wenyewe. Ninawahitaji, wananifurahisha, napenda sana kuwa mwenyeji wao. Kwa hivyo, nilijiunga na Mkusanyiko wa Ubuntu mara nyingi kadri nilivyoweza (na bado ninasikitika kuwa ilibidi nikose chache!) Kwa sababu nilifurahia tafakari yaaminifu ya wazi ambayo tulihimizwa tuzingatie. Niliona kama inaburudisha, haswa wakati ambapo mitandao mingi ya wavuti ilihitajika eti tuonyeshe utaalam wetu. Kulikuwa pia na mchanganyiko mzuri wa machozi na kicheko, kuandika na kucheza densi, kutulia na kusongasona. Kuna kipi cha kutopenda?

**Je, Mkutano huu wa Ubuntu umekusaidiaje kwenye safari yako ya uponyaji?**

FM: Nimekuwa kwenye kizuizi madhubuti kwa miezi mitatu moja kwa moja na familia yangu, na ingawa ninajua kabisa kwamba nimekuwa kwenye nafasi ya fadhila bora zaidi kuliko wengine kuweza kukumbana na hali hii na kujilinda kwa njia hiyo, mimi kama ambaye ni mndani wa kutosema sana nimekuwa nikipambana na ukosefu wa huo muda wa unyamavu na utulivu wa kutafakari pekee yangu. Kuongezea kwa hayo, wasiwasi niliokuwa nao juu ya kila mtu ambaye makazi yao hayakuwezekana au yalikuwa hatari, na kisha ukumbusho wa kikatili kwamba ulimwengu bado ni mahali penye ubaguzi wa rangi… tuseme kutunza afya yangu ya akili imekuwa changamoto. Mkutano wa Ubuntu umenipa nafasi kwa jamii, tafakari na furaha. Ninashukuru sana kwa hilo.

# NDOTO ALINACHA ZA DEMOKRASIA REHANI

Raquel Lima, Portugal/ Angola



**Demokrasia ni wazo lililobadilishwa kuwa bidhaa na huduma,
Zanunuliwa na akiba ya fedha, zanunuliwa na karibu bure.
Zanunuliwa kwa imani ya kuwa ni biashara isiyoegemea maslahi,
Ya kuaminika, isiyoweza kubadilika, na iliyo na dhamana isiyo na kikomo.**

**Hatimaye, ilitokea kuwa ni mkopo uliokuwa amana kwa ubepari,
Ya muda mfupi, yenye mfumuko wa bei, ya kuvuta riba, na kuelekeza hadi kuzimu.**

**Mtaji ni utajiri uliyozalishwa, kulimbikizwa na kuekezwa tena,
Kipindi ambapo umma ulitumainia usalamamali wa kijamii:
Walilipa kodi zao, na walitozwa ushuru, wakalipa tena, na wakatozwa tena,
Walituzwa haki zao za kibinadamu, ila kama mitambo.**

**Kwa kuzingatia mifumo yote iliyoko, ule wa kidemokrasia ukawa ndo wa haki na madhubuti zaidi.
Sarakasi nzima ya kisheria iliyoinuliwa kwenye bendera iliyopeperushwa angani,
Na sisi tukaifuata, Imani yetu ikilenga hilo suluhisho,
Huku katika ndoto zetu tukitumai ya kwamba demokrasia, baadaye, haitawekwa rehani.**

**Lile jumba kuu likiwa na baadhi ya vifaa ambao ni mkusanyiko wa rafu
Zilizojaa mifumo ya haki, uchumi, fasihi, sanaa na ushenzi
Ubinadamu, mada za kijamii, sayansi, elimu
Na katika kila mojawapo, tulihakikishiwa ya kwamba, kulikuwa na uhuru wa kujieleza.**

**Wenye ngozi nyeusi, kila wanakofanya kazi, wamekema kwa muda ya kwamba hakuna demokrasia.
Hawachukuliwi kama binadamu, ila rasilimali na bidhaa za biashara.
Kwa hiyo wakaonelea waongezee safu zingine chache mle jumbani:
Biolojia, rasilimali watu, anthropolojia, kutangulia.**

**Ila kuweza kuuza demokrasia kulihitaji uwekezaji mkuu,
Kutuuzia njozi ya kwamba tunajidhibiti wenyewe kikamilifu
Na kuandamiza pamoja na kukomesha kabisha wazo la kujikomboa
Ili ndiyo mabenki, mipaka na makanisa viweze kuchukua mahali pa wokozi.**

**Lile jumba la ukandamizaji lilikuwa jirani na jumba la ufashisti.
Majumba yote mawili yakidumisha jumba kuu la kale la ubepari.
Ili kurehani demokrasia - - mipako mine ya rangi safi,
Badilisha milango na makufuli, zifiche droo kwenye dari.**

**Kupaka rangi eneo la kuonekana la mbele ya jengo ilikuwa ndo kazi ngumu zaidi.
Hata wale wa chama cha Republican na kile cha Democrat waliwasili kusaidia!
Ila mavazi mazuri yalikuwa yanaonyeshwa kila wakati
Wakatoka kulia kuelekea kushoto wakituzomea na wagombea uchaguzi**

Huku majumba yaliendelea kunawiri kidemokrasia
Hivi kwamba sio wengi waliweza kuipata harufu ya uvundo hewani,
Uliokuwa na harufu ya mauaji ya kimbari: Wayahudi, Jamii Asilia, Weusi na Wazururaji,
Lakini tukirejea mle jumbani walikatika miziki ya Fado, Flamenco na Tango

Demokrasia... wazo lililobadilika na kuwa bidhaa na huduma,
Lililonunuliwa kwa akiba ya fedha, lililonunuliwa kwa bei ya karibu bure.
Lililonunuliwa kwa imani ya kuwa ni biashara isiyoegemea maslahi,
Ya kuaminika, isiyoweza kubadilika, na iliyo na dhamana isiyo na kikomo.

Hatimaye, ilitokea kuwa ni mkopo uliokuwa amana kwa ubepari,
Ya muda mfupi, yenye mfumuko wa bei, ya kuvuta riba, na kuelekeza hadi kuzimu..

Na kila mmoja alijua ya kwamba ulafi na majivuno
Walikuwa tu ni dada wadogo zake Bi Ukoloni
Hata hivyo, waliendelea na kununua demokrasia
Bila kufahamu, bila hatia na kwa ukaidi.

Na kama kungetokea yeyote mwenye ujasiri wa kusema lolote kuhusu ongezeko la joto ulimwenguni,
“O, hayo tu, upumbavu ulioje, ni hali ya dunia, ni tukio la kiasili,”
Inanuka kama dioksidi ya kaboni, magesi na nyumba za vioo,
Mafuta ya kinyesi yaliyoteketezwa na misitu mvua ya kitropiki

Miaka ya sauti zilizonyamazishwa: miaka ya demokrasia
Miaka ya maisha yaliyoharibiwa: miaka ya demokrasia
Miaka ya wanawake kunajisiwa, kuhamishwa, kuingizwa kwenye utumwa: Miaka ya demokrasia

Miaka ya ujasusi unaowalenga waasi wanaopinga kupatikana kwa uhuru
Ilivunda kama wanamgambo, kama shutuma na nadharia za kimapinduzi
Na hapo ambapo yale yaliyodhaniwa kuwa siri yalinyonya na kumaliza bajeti
Kisha mweledi mmoja wehu akavumbua mitandao ya kijamii

Kwa sababu kwenye ulimwengu huu wa kidemokrasia tutaweza kushiriki
Taswira ya maisha yaliyotimika, na yale yote tuliyoyaota:
Itikadi mbalimbali, vyama vya kisiasa, kule tunaposafiri kwa likizo yetu,
Sanaa, magari, mitindo ya maisha na kila kitu tunachopangia,

Wala si chochote kuhusu kujitolea kwetu kwenye sinia,
Yale ambayo umma hutafakari na watu wanatamani,
Cheri juu ya keki bila wasiwasi wowote:
Mtandao wa intaneti ukiamuru ni yapi ya ukweli, historia au ya kubuni

Demokrasia…dhana iliyobadilishwa na kufanywa kirusi,
Ikinunuliwa kwa akiba, ikinunuliwa kwa dhamani inayokaribia bure.
Ikinunuliwa kwa dhana ya kwamba ina thamani kubwa.
Ila kwa maslahi gani? …ilikuwa ni vita vikuu vya tatu vya ulimwengu.

**Limetafsiriwa kutoka lugha ya Kireno na: Martin Earl **

# SHAJARA YA TASWIRA-HADITHI NA TAFAKARI ZA MSANII KATIKA KIPINDI CHA COVID-19

*Nancy Chela Cherwon, Kenya*



Kwa wakati huo, nilikuwa nia mazowea ya kutoka nje ya nyumba na kuketi pale ili kuweza kuisikiza tu miti na ndege na kujaribu kutofikiria mawazo ambayo yaliokuwa yakinitatiza haswa kwa wakati huo. Hili lilinisaidia sana kuweza kushinda wasiwasi wangu na matatizo yangu. Hadi kufikia sasa, mimi hujihusisha katika Uwazo ili kujikumbusha mwenyewe binafsi kama mimi ni nani na safari yangu kama msanii, na hata pia kama tu kiumbe kingine chochote humu ulimwenguni.

## UZITO WA DUNIA

Kwangu mimi, uwazo ni kutazama ndani siyo kwa kutaka kuhukumu ila kwa mtazamo wa upendo na utunzaji. Uwazo kwa maoni yangu ni hali ya kuyajali mazingira yako… pale unapoishi, wale watu ambao una muingiliano nao, na pia kutazama kila kitu ambacho kiko nje ya nafsi yako lakini kwa njia moja au nyingine inakufafanua wewe.

Uzito wa Dunia au almaarufu Weight of the World ni mchoro unaoonyesha mwanamke aliyeutwaa ulimwengu mkononi mwake kwa njia ya uangalifu wakati ambapo anaendelea na tafakari au uwazo. Lengo ni kuashiria ya kwamba kupitia uwazo anapata uwezo wa kutenda lolote ambalo moyo wake unapenda.


Hili ni kumaanisha ya kwamba: “umeubeba ulimwengu wote mikononi mwako”.

Hii inalenga kutuhimiza ya tuweze kujiamini kama viumbe visivyoweza kuzuiliwa. Hata hivyo, ni nani huweka vikwazo au vizuizi?

Vizuizi vyote tunavyovijua duniani viluwekwa na mume, na si vyote vilivyoundwa kutoka kwa nyenzo sawia.

# Sharaja taswira ...

*msaani Nancy kuhusu uchoraji wake ambaye ni picha kuu la Marisa... hili.*




## UHURU

Utunzi huu unaoitwa Uhuru haswa unahusu safari ya kutafuta nafsi... kuwa na uhuru kutokana na mashaka na taabu za humu duniani. Anga na nyota zinaashiria uhuru huo. Ni ishara ya hali ya Amani na uhuru na anavyoelea kwa utulivu. Manukuu yaliyoelekezea kwa kuanzishwa kwa kazi hii yalikuwa ni:

*"Lakini subiri, hapa pana utulivu ulioje. Je, naweza kuwa huru, kuna uwezo wa mimi kuwa mimi... Je, ninaweza kuwa Chelwek."*

Nilirekodi manukuu haya siku moja usiku wa manane mnamo kipindi hiki cha ambo. Nilijihisi tu ikinwa na dhiki, nikiwa nimepotea na sina hamu ya kufanya kazi yoyote haswa muda huo.

Kwa wakati huo, nilijihisi kama kwamba nilichotaka ilikuwa ni kuelea tu nikienda zangu... niwe mimi binafsi bila wasiwasi wowote wala kujali chochote hapa ulimwenguni. Nilijihisi nikiwa huru, nilijihisi kwamba nilikuwa na ule ukweli kwa kule kuwepo kwangu, na nikawa na hisia ya kwamba yote yalikuwa yanawezekana katika nafasi hiyo na wakati huo.

Kwa hivyo nikaamua kukibandika jina kipande hicho cha sanaa na kukiita - Uhuru.. Utunzi huu unatusaidia ili kujitahidi kupata uhuru kutokana na maradhi ya COVID-19 kwa sababu ni ukumbusho tuweze kutafuta ndani... uweze kujipata mwenyewe binafsi katika nyakati hizi za dhiki...

**USIRUHUSU WASIWASI ULIO NJE YA NAFSI YAKO KUWEZA KUKUONGEZEA UZITO KWA SABABU SISI TUNA NGUVU ZAIDI YA AMBO HILI...**

*na daima TUTAENDELEA KUIBUKA.*

# MAONI NA MANDHARI....

## MAHUSIANO: MAMBO ZA KIROHO, MATUMAINI AND UPONYAJI





# Waponyaji ni kina nani?

Na Fatime Faye, Senegal

Tangu wakati wa zamani za kale, Waafrika wametumia mbinu mbalimbali za uponyaji, njia ambazo zilipokelewa kutoka kwa utajiri mkubwa wa tamaduni za Kiafrika, mila, desturi na aina tofauti za mimea na wanyama… njia ambazo zilifanikiwa na kuendeleza jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine hadi wakati wa ukoloni na ukoloni mamboleo. Lo! Nitaachia hapo kupoteza mkondo… Hayo yatakuwa mazungumzo kwa siku nyingine. Kwa hivyo, ni nani Waponyaji wa Kiafrika na ni jinsi gani Wanawake wa Kiafrika wanaweza kurudisha mila na mazoea yetu ya uponyaji wa Kiafrika?

'Mimi singependa kujitambulisha kama mganga wa uponyaji. Mimi ni mwanamke wa kawaida ambaye hutumia maarifa yake kusaidia marafiki, familia na jamii."

Ninatumia mbinu za kukanda mwili ambazo nilijifunza kutoka kwa bibi yangu kuponya homa wakati watu wana ugonjwa wa malaria – mojawapo ya njia nyingi kama wanawake wa Kiafrika tumepitisha mwali kwa wanawake wengine kupitia njia mbalimbali za kielimu. Jina la ukandaji mwili huu ni "damp". Inafanywa kwa watoto baada kidonda cha kufungwa kitovu chao kupona. Ni ukandaji wa mwili laini na wa kupendeza na chembe kidogo za maumivu hasa katika mwisho wa ukandaji wakati mtoto ameshikwa kichwa chini na kutikiswa kidogo. Mwanzoni ukandaji mwili unamshangaza mtoto na kulia kwa maumivu. Baada ya kunyooka zaidi, mtoto huishia kuutarajia ukandaji mwili huo na kuupenda. Ukandaji huu siufanyi kufurahisha bali "kuponya" na wakati mwingine kujua maumivu yanatoka wapi. Ikiwa unamkanda mtu ambaye ana ugonjwa wa malaria inayoathiri neva kwa njia hii, wakati unamkanda kichwa, mtu huyo atalalamika kwa kuwa na kizunguzungu kikali.

# Waponyaji ni kina nani?

Njia ya pili ya uponyaji ambayo mimi hutumia inaitwa "**mocc**". Unaweza kuona moja ya mbinu zake katika nyingi za ukandaji wa kiasili. Kwanza, weka mkono wako kwa muda mfupi kwenye sehemu inayougua ya mwili na kisha uchukue na kutikisa ile "hatari", kiwewe ama sumu au hata kitu chochote ambacho watu wanapendelea kukiita ili kitokee mikononi mwako. Mbinu hii inatokana na imani ya kwamba ugonjwa hutokana na hali za aina mbalimbali za kiwewe (za kiroho, za mwili au za kisaikolojia). Watu wengi huugua miezi mitatu hadi sita baada ya kufiwa na wapendwa wao au wamepitia katika matukio ya kuleta kiwewe. Wazo ni kuondoa maumivu kutoka kwa mwili kwa njia ya "**mocc**".

Wakati mwingi, unapoanza, utahisi na mikono yako kwamba sehemu ya mwili inayougua ni ya joto la juu la mwili zaidi ya sehemu zingine – joto kidogo, joto la kadiri hadi joto sana. Ninamalizia sehemu ya kwanza ya uponyaji wakati mtu anasema kwamba yeye husikia bora au wakati joto linapunguka sana. Halafu mimi hufanya mtu afikirie juu ya sufuria ya mtindi ambayo umechota kijiko cha yaliyomo.

Sehemu ya pili ya uponyaji ni kujaza sehemu inayokosekana na matamshi mazuri na maarifa yaliyomo ya uponyaji. Mchakato wote unategemea imani kwamba mtu anayefanya mila hiyo ni mfereji / chombo / njia ya mawasiliano kati ya mtu huyo na vyombo vingine (waponyaji ni vyombo vya kiroho ambavyo watu wengine huvitambua wazi au huenda wasitambue). Wakati wa mchakato mzima na baada ya hapo, unasikia wasiwasi na unashukuru vyombo hivyo:

"*Wahenga, tafadhali nisaidie kuponya* (jina la mtu huyo)". "*Ahsante kwa kunisaidia kuondoa kiwewe kutoka* (jina la mtu huyo)".

Unapomponya mtu na ugonjwa mbaya, tafadhali osha mikono katika maji yenye chumvi hadi kwenye kiwiko chako kabla na baada ya ibada.

Ya tatu ni ile ya kisasa inayoitwa Tiba ya Kutoa Hisia za Kihemko, almaarufu "**Emotional Feeling Relief Therapy** (EFT)" au Tiba ya kugonga polepole, almaarufu Tapping Therapy. Wazo ni kugonga sehemu fulani za mwili na kurudia sentensi: "Hata ingawa nahisi huzuni (au hisia zingine chungu), najipenda sana na ninakubali mimi ni nani". Inayo mbinu mbadala ambayo ni kuweka mkono wako kwenye kifua cha mtu na muombe mtu huyo atoe rangi kwa hisia na kuiruhusu iende kwenye mkondo (kutoka kwa fikira). Mimi kawaida husema baada ya rangi kuchaguliwa: "Ona picha kama ni mkondo na uiruhusu itiririke kupitia mkono wangu. Haitaniumiza kwa sababu ninaitikisa mara kwa mara mikononi mwangu kama hivi". Nami namwonyesha ishara ambayo ni sawa na ishara ya "**mocc**".

# Waponyaji ni kina nani?



La mwisho, sina uhakika na jina lake. Niliichukua wakati wa kikao cha uponyaji kutoka kwa mganga (The Noble Touch). Hii ibada unayofanya baada ya kusafisha mwili kwa kutumia ile mbinu ya Kugonga Polepole au EFT. Unauliza mtu unayemponya: "Fikiria kuwa una bakuli la kioevu juu ya kichwa chako. Kioevu kina rangi nyepesi na nzuri. Unaisongeza bakuli kwa upole ili kioevu kinamimina na kujaza kichwa chako. Macho, mdomo, kidevu, shingo, n.k. Halafu, koo, kifua, moyo, n.k., kisha nyongo, viungo vya ngono, makalio, miguu, miguu na kumwagika ardhini ". Unaweka ndani ya kioevu vitu vyote unavyohitaji: furaha, afya, upendo, n.k

Mila hizi zote za uponyaji zina vitu viwili vinavyofanana. Kutoa sauti na wazo kwamba sote tunaweza kujiponya wenyewe kwa mikono yetu na hata hali tunayoiunda ya kiakili. Tumepoteza tu uwezo huo kupitia njia hiyo. Unapojigonga kwa nguvu na kujiumiza kwa kidude chochote kile, jambo la kwanza unalofanya ni kushikilia sehemu ya mwili wako inayohisi huo uchungu. Hili, huponya. Weka mkono wako tu kwa makusudi huko na utumie akili yako na ujiponye mwenyewe! Ni rahisi na karibu kila mtu anaweza kuifanya kwa kibinafsi au kwa watu wengine.

**Waponyaji ni kina nani? Waponyaji ni watu ambao wanapenda sana watu wengine: marafiki, familia, jamii na ulimwengu wote. Upendo huponya na husaidia kuponya mateso.**

Unapokuwa mmoja wa watu hao, tafadhali jisikilize mwenyewe au ishara ambazo hukuambia nini cha kufanya. Labda umekuwa ukifanya hivyo kwa muda mrefu bila hata kufikiria juu yake. Wengine wanakumbatiana, wengine huimba, wengine hucheza densi, wengine huomba, n.k. Kaa na ufikirie juu ya mara ya mwisho ulipokutana na mtu aliye kwenye maumivu. Ulifanya nini? Je! Mtu huyo alisema: "Nimepata nafuu"?

Mwamini yeye/wao.

Wewe ni mponyaji.

Sisi sote ni waponyaji

# *Mawazo na Maoni kutoka kwa Mponyaji mwenye kufuata mienendo ya kiafrika na mtawa*

**Na Dada Letta Mosue, South Africa**

Nawasalimuni nyote kutoka Afrika Kusini.

Niko hapa kuwapa ujumbe wa mshikamano, msaada, kupeana matumaini na kuwatia moyo wanawake wengi wa Kiafrika wanaoteseka wakati huu wa janga la Corona ili kuwaunga mkono, kiakili na kiroho ili kujipatia nguvu zaidi, kustawi na kuwa hodari zaidi. Mimi niko hapa kudengua: "Umuhimu wa kuzingatia sio tu kwa afya yetu ya mwili, lakini pia kwa ustawi wa kiroho".



Hautaniamini nikikuambia kuwa, sina shida ya ugonjwa wowote ule sugu. Ni wakati tu nikijishughulisha sana na kazi mfumo wangu wa kinga "toi-toi" (hupakia juu) na mimi hupata mafua. Siku mbili za kupumzika ni za kutosha kunirudisha kiafya kwa msaada wa dawa ya "granny's raad" (ushauri wa bibi), ambayo ni, matumizi ya mimea ya dawa au asili. Jinsi ninavyoshughulika na mafadhaiko ni kutumia "bomba-bomba" ambayo ni EFT (Mbinu ya Uhuru wa kihemko) ambayo huwafundisha wateja wangu ambao wamepata kiwewe au hawawezi kulala vizuri usiku.

Walakini, jumla, kwa kuwa nilikumbatia zawadi ya babu yangu ya uponyaji katika damu yangu, nina amani ya akili. Ninafanya ibada ikiwa ninahitaji. Kwa haya huwafanya pamoja na familia yangu nyumbani. Ninaomba na babu zangu ambao ninawaalika kuungana nami wakati wowote ninapoomba sala za Kikristo. Sijisikii nikiwa peke yangu au mpweke hata ninaposafiri kwa sababu ninawaomba (mababu zangu) waambatane nami.

***Mimi pia niko hapa kuhamasisha wanawake wengi kwenye bara hili ambao imani na hali ya kiroho ina maana sana kwao kama urithi wao wa Kiafrika.***

# "Ninaombea Afrika ipate tiba ya gonjwa hili na sio kuwashinda wale wanaotutazama sisi watoto wa bara hili.."

Kwa mzozo kama huu na ukubwa wake; Corona imetuonyesha kuwa ina uwezo wa kuwa na athari kwenye nyanja zote za maisha yetu; pamoja na imani, hali ya kiroho na jamii ya wanawake wa kiafrika ambao wanafuata dini yao na uponyaji. Ingawa sina ushahidi wa kweli, lakini ninachoweza kusema ni kwamba ikiwa imani yako inategemea kukutana na watu wa dini yako na sasa lazima ukae nyumbani, umbali wa kijamii, kujitenga, imani yako lazima iathiriwe, hii haipaswi kuwa ya kudumu. Ninapenda katika bibilia ambapo Yesu Kristo alimwambia yule mwanamke Msamaria: "Wakati utakuja ambapo hamtaabudu juu ya mlima huu au kule Yerusalemu, mtaabudu kwa akili na ukweli". Kama hivyo, kwangu mimi kuabudu kutoka moyoni kwa sababu ya vikwazo vinavyoletwa na sharia za corona hasa mikusanyiko ya kijamii ndio hufanya maneno ya Kristo kuwa ya ukweli leo. Kiroho kwa upande mwingine, ikiwa ni Imani ya kweli haitegemei ikiwa unaabudu kwa ushirika au dini gani. Imani hutufunga kote kwa dini na ndiyo inayotusaidia kukabiliana na janga hili. Hisia na Imani zetu hutupa tumaini wakati wote.

Kwa kawaida, watu huuliza: 'Dada Letta, unawezaje kuwa Mponyaji Mkuu na Mtawa wakati huo huo? Au unawezaje kubeba kofia zote mbili na kwa neema hiyo? ' Jibu langu kwa watu ambao huuliza swali hili ni "Mimi sio dhiki". Ndani ya muktadha wa Kiafrika hakuna uwezekano wa binadamu kuingiana kwa undani. Yetu ni mambo ya kiroho kamili. Ni kwa sababu hii kwamba watu wana shida na mimi kukubali kipaji cha uponyaji wa babu yangu na kuwa mtawa, lakini sijisikii au kuhisi mgawanyiko tena. Hapo mwanzo nilijitahidi kwa sababu ya pande mbili za tamaduni ya Magharibi. Ilikuwa ni dhidi ya au kwa ajili yangu, lakini sasa niko nyumbani kwenye ngozi yangu. Swali langu ni: Je! Kwanini niwe Mkatoliki wa Kirumi na sio Mkatoliki wa Kiafrika?

Hii inanifanya kushuku na kutoamnini jinsi tunavyokubali na kuamini matibabu ya Magharibi na uponyaji kwa gharama yetu. Tunapaswa kusikitishwa kwa sababu dawa ya Magharibi inaiba mimea yetu ya kiafrika, kuweka vihifadhi na kuiuza barani Afrika kwa bei kubwa. Napenda kuwapa changamoto wanawake wa Feminist Republik kufanya utafiti na kurejesha urithi wetu wa uponyaji. Huu ni wakati. Tunahitaji kuunga mkono watafiti na wanasayansi wetu wa Kiafrika ikiwa hatuna vipawa vya kusoma mimea ya kiafrika na kutoa dawa ya uponyaji wa asili na chapa ya Kiafrika. Kuna wazee wengi katika vijiji vyetu walioponya wagonjwa kwa kutumia mimea. Wacha tuende huko kuongea nao na kujifunza kutoka kwao.

Songa mbele; tunapojiweka katika nyakati ngumu na zisizo na uhakika hizi, wanawake wanapaswa kujenga nguvu zao za kiroho. Mtu angeuliza vipi? Kwa kuja pamoja kufanya ibada na kushiriki maarifa juu ya mwito kuwa mponyaji na ujuzi wa mimea na miti ya dawa. Mimi niko katika sehemu ya kikundi kinachoitwa Sangha Circle kilichojumuisha
waganga wa kiume na wa kike waliopitia siku 21 za safari ya kuanza mtandaoni.

Ninapowaaga, kumbuka haya mambo muhimu ya kuzingatia mazoezi ya kiroho:

- Usiombe msamaha kwa mtu yeyote au dini yoyote kuwa wewe ni nani au kuwa na imani ya kiroho chako cha Kiafrika.
- Usiwafedheishe mababu zako kwa kuona aibu kuhusu kipaji cha kuwa mponyaji.
- Jivune na utembee kwa madahabea mrefu kuwa 'wewe ni mtoto wa ulimwengu na unahaki kuwa haha.'

# hatarishi:

Limetungwa na Joia Sabimana

kivumishi

1. siyo imara au thabiti; inaweza kung'oka au kuharibika / kuvunjika.
2. *(kuhusu mtu) kutokuwa na uhakika au kuwa na wasiwasi kuhusu hali yake binafsi; kukosa kujiamini.*
   *Visawe: kutojiamini mwenyewe, kutokuwa na hakika, kujitili shaka mwenyewe, kujitilia vikwazo, mwenye uwoga, kutoweza kuwa na starehe*

Mara hii uwe mzuri kwangu.

Uliondoka kwenye hema letu takatifu muda mrefu uliopita, ukaniambia unaenda kupambana na vikosi ambavyo vilikuwa vimetangaza vita dhidi ya miili yetu. Vitisho kwa wale wa aina yetu vilikuwa ya kwamba hakukuwa na lolote ambalo ningeweza kufanya ili kukushawishi usiondoke. Kwa hivyo nikakuimbia wimbo, nikakupatia mwanga wa macho yangu, na kukusindikiza kwa maneno ya fadhili. Usiku kila siku, na wakati mwingine unapouona uso wako ukionekana kwenye kioo, unaonja ladha kidogo ya sura yangu...yetu, tukigundua ajabu katika hema letu la siri, pamoja. Lakini ulienda kwa kitambo kirefu sana nikahofia huenda janga tu ndilo litakuregesha kwangu.

Hivyo vita vilikufanya kuwa shupavu. Miili mingi sana iliyo hatarini, na najua kwa hakika jinsi ambavyo moyo wako unavuja damu kwa kila mojawapo ya miili hii. Kuilinda kwa gharama yoyote, siyo?

Vita hivyo vilikufanya ukasahau njia za upole, za mapenzi ya kweli, za uhusiano wa karibu ambao hauna kuambatana katika hali hatarishi. Ulisahau kujitunza binafsi, pendo.

Nilijua utarudi kwangu siku moja, kwa hivyo nilipanga pawe na nafasi yetu kuketi, pamoja na mawazo machache kwako uweze kutafakari kwenye safari yako ya kutafuta kujipenda na uponyaji:

*Kwa hivyo walidhani wangeweza kukuvunja*
*Wakurai kuucheza mchezo wao, ujikunyate chini ya mkono wao wa chuma*
*Lakini hawawezi kulikunja bahari, au siyo?*
*Au kuiambia volkeno irudi usingizini wakati inapoamka...*
*Bila shaka wanachukizwa kila unapojitetea mwenyewe binafsi*
*Kwao wao, hapapaswi kuwepo nafasi ya Nafsi.*

Unapoanza kuiweka Nafsi yako katikati, mara kwa mara utahisi kana kwamba haufahamu unalofanya. Utahisi kama ni tendo la kigeni, hilo tendo la kujiwekea macho ya upole kwako mwenyewe binafsi na kuangalia ukamilifu wa utu wako wote ukibubujika na kutiririka na kufungamana wenyewe na Ulimwengu.
Usiondoke.
Kaa hapo kwa muda.
Ufanye mwili wako kuwa hekalu. Na humo ndani ya hekalu, fanya mazoezi ya maumbo mengi ambayo inawezekana kwa Mapenzi na Maisha, hadi pale utakapoweza kukumbuka kwamba ile lugha ya mwili wako ndiyo lugha ya Ulimwengu.

Nitakuwa hapo pamoja na wewe, daima.
Na mapenzi yasiyo na kikomo,
Wako mwandani Msichana Mweusi <3



# KUPATA UPONYAJI KATIKA UPENDO

NA ELIZABETH OMBATI

Najirusharusha na kugeukageuka kitandani. Nikiibembeleza Roho yangu ijisalimishe kwa Usingizi. Lau kupumzika kwa muda tu. Kesho itakuwa ni siku nyingine ndefu. Naunyoosha mkono wangu, na kuifikia simu yangu, labda si busara kufanya hivyo. Kwa sababu huenda nikajipata kuzubaa kwa masaa mawili yajayo, nikidadisi ni yapi yanaendelea karibu na mimi, usiku huu. Huenda nikapotea huku nikibingirisha kupitia ratiba za nyakati kuona ni nini kila mmoja anasema kuhusu janga hili. Jinsi wanavyohangaika kupata usingizi, kama mimi tu. Natazama saa tena, inaelekea saa nane usiku. Hali hii huenda iendelee hadi saa kumi alfajiri. Je, niendelee kujilaza tu hapa hivi bila usingizi? Akili yangu itarandaranda hata zaidi, huku nikiwaza uwezekano wote uliopo duniani, hadi pale ambapo, kwa hiari yake mwenyewe, usingizi utanizuru na kunipeleka?

Ninauwasha mtandao wa Youtube. Ni ipi njia rahisi zaidi ya kupata usingizi? Labda nijaribu kucheza muziki wa uwazo. Kuna aina nyingi sana ambazo naweza kuchagua, kuna zile ambazo zinaahidi kukupa usingizi baada ya dakika tatu. Nachagua huu muziki, na kujipeleka moja kwa moja hadi sehemu ya maoni. Dakika tatu zinaisha hivyo tu, na nina hakika ya kwamba hili halitawezekana kamwe. Labda ni bora niamke tu niweze kufanya kazi kwenye kompyuta yangu hadi pale ambapo usingizi utanipata, wakati utakapoamua, au siyo?

Ukweli ni kwamba nianishi na matokeo ya utambuzi wa maradhi kwamba nina tatizo la wasiwasi, na hili huenda limeathiri zaidi hali yangu ya sasa. Akili yangu imo kwenye mashindano ya mbio, na ni kila wakati, huku akili ikijaribu kubaini yote yanayoendelea katika ulimwengu wangu. Je, kuna uwezekano wa haya kuisha hivi karibuni? Tutaweza kurejelea siku za hapo awali, enzi ambazo hakukuwa na haja ya kubabaika kuhusu kusitishwa kwa shughuli na kuwepo kwa ratiba ambayo kwa njia moja au nyingine hairuhusu uhuru wa kibinafsi hata kidogo? Ninao ufahamu, katika mawazo yangu ya ndani, ya kwamba huenda natumia muda na rasilimali nyingi zaidi kwenye mitandao, zaidi ya muda ninaofaa kuutumia, lakini, je, nina mbinu gani nyingine ya kuweza kujiunganisha na upatikanaji wa uponyaji? Kuweza kujiunga na usaidizi?

Wiki jana nilikuwa kwenye kundi la mtandaoni la usaidizi wa mahirimu na, Mungu wangu! Si nilifurahia sana huo muda wa masaa matatu ya kuungani na wenzangu. Tuliweza kusogeza kuhusu kila kitu, uoga wetu na matumaini yetu.

# Uponyaji katika Upendo....

"Yale yaliyotufanya tucheke na yale yaliyotufanya tulie. Tulizungumza kuhusu furaha ambayo tulikuwa tumeitamani kwa muda mrefu, na tamaa yetu ya kurejelea hali ilivyokuwa ya kawaida. Tulipendana sote kupitia kwenye mtandao. Tulipata uponyaji. Ninatamani kikao kitakachofuata na kile kingine kitakachofuata. Huenda labda, janga hili bila shaka, lina jambo ambalo linatukumbusha kuhusu yale ambayo huenda tunapokonywa kwa sababu ya ulimwengu wetu ambao umejaa shughuli nyingi hata tukakosa muda wa kujijali..."

Ulimwengu wenye shughuli tele ambamo kila mmoja wetu yuko mbioni kupita huku na kule, tukitafuta Uradhi na upendo, tukitafuta jinsi ya kutimiza ndoto zetu ila badala ya hiyo tunakumbana na mafadhaiko katika juhudi zetu hizo. Maisha ya mashindano na ya haraka. Hivi kwamba wakati mwingine hatuna muda wa kukatiza ili kupata mapumziko. Huenda ikawa ambo hili linatukumbusha sisi, hivi kwamba kwa sasa kwa vile tuna muda zaidi kwa kuwajali wenzetu, muda zaidi wa kudhihirisha hatari tulizomo sote kwa wenzetu, muda zaidi wa kupendana, hata ikawa ni kwa umbali; huenda ikawa ulimwengu unatukumbusha sote ya kwamba, tusije tukasonga mbali zaidi kutoka kwa roho ya urafiki na mapenzi. Kwa sababu mapenzi ndiyo nguvu inayotushikamanisha sisi sote pamoja kama binadamu.

Nguvu za Mapenzi. Sisi tungekuwa wapi bila mapenzi? Nakumbuka kama ilivyokuwa vigumu sana mimi kuweza kushikilia ajira zangu miaka kadhaa iliyopita. Wasiwasi sio kitu kizuri. Ila sasa pia nakumbuka jinsi ambavyo mapenzi yamenitoa mbali na kunifikisha hapa nilipo. Mapenzi hufukuza uwoga, mimi ninafahamu, kwa undani na kina zaidi.

Ndani katika Roho yangu nafahamu ya kwamba hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kunawiri bila Mapenzi. Ninaamini ya kwamba Mapenzi ndiyo yanayoleta maana katika maisha yetu. Hivi niweze kusea nini, eti kandarasi yangu ya kazi iliisha mnamo mwezi wa Machi, pale ambapo ndiyo tulikuwa tunaanza kuingia katika kipindi cha kuzuiliwa uhuru wa kufuata shughuli zetu zote za kawaida. Pale tu ambapo tulikuwa tunaanza kuwa na uzoefu wa maisha kama jinsi ambavyo hatujawai kuyaona wakati mwingine hapo awali. Vitega uchumi vilikuwa vinapotezwa, ajira, na kila mahali kulikuwa na wasiwasi mwingi ukizidi kutanda, je, siku za usoni zitakuwaje?

Na nilisalia nimeshikilia Mapenzi, nilijua ya kwamba Mapenzi yataweza kunisitiri na kunifaa. Hapo jana tu nilipata fursa ya kuhudhuria mahojiano ya kazi. Inaleta hisia kama ile ya kufikia kwenye sehemu yenye maji na rotuba katikati ya jangwa kubwa, ishara ya Matumaini. Ule mmea wa rangi ya kijani wa dungusi kakati, unaopatikana baada ya muda mrefu wa kutafuta na kutafuta bila kuchoka, lakini ishara ya mmea huu inaniarifu ya kwamba kuna matumaini. Kuna maji. Hatutakufa kwa sababu ya kiu.

Ninaweza kuhisi, kwa mbali ishara kidogo ya usingizi. Natumai ya kwamba hivi karibuni au baada ya muda usiokuwa mrefu sana Roho yangu hatimaye itaweza kupumzika. Labda hata Niote. Na niwe na wingi wa matumaini ya kuiona siku nyingine, iliyojaa ndoto na matumaini, na Mapenzi.

Mapenzi. Naomba upendo uweze kuijaza mioyo yetu kwenye vipindi kama hivi. Mapenzi ya watoto wetu. Mapenzi ya Wapenzi wetu. Mapenzi kwa kazi zetu na ajira tulizopangia, mapenzi ya sanaa na urembo. Naomba Mapenzi yatusaidie kuyamudu maisha yetu, kufahamu ya kwamba hata wakati ambapo tunajihisi tukiwa na upweke mkubwa, Mapenzi huwa hayaondoki. Huwa yupo hapa, ametukumbatia karibu sana na moyo wake. Na anatuambia sisi, 'usiwe na shaka. Ndani yangu mimi unapata uponyaji wako.' Na ni ukweli kabisa, kwa sababu mimi nilipata uponyaji wangu ndani ya Mapenzi.


ULIMWENGU USIO NA MIPAKA
YA SANAA KWA WOKOVU
ULIO WA
KWELI NA USALAMA
NA AMAL HAMED

# Tulipatana na msanii Amal kuongea juu ya kazi yake anayoiita "Hisia"




## Je, tueleze kiasi juu ya hii usanii 'Hisia'? Pia kuna vile vikundi vya wasaani na watetezi wameungana kukabiliana na shida hili la janga kubwa?

Mchoro uliochaguliwa ni matokeo ya safari ya kibinafsi iliyoanza mnamo 2017, lakini siwezi kabisa kutenganisha safari yangu ya kibinafsi na kile kinachoendelea kunizunguka kwa sababu msanii ni mchanganyiko wa maisha ya umma na ya kibinafsi - nakama binadamu anayetetea haki za binadamu wa kike ninakubali kabisa kuwa 'Ubinafsi ni jambo la kisiasa'. Msanii pia huathiriwa kila wakati na mwingiliano na wasanii wengine kupitia uwepo wake kama mtu ndani ya kikundi au pamoja, ndani ya jamii ambazo alilelewa na mahali anakoishi sasa. Kile tunachozingatia kama matokeo ya safari ya kibinafsi pia ni matokeo ya safari katika nafasi ya umma. Safari hii ni safari ya kujitambua na jinsi ya kutumia sanaa - kwa kila aina - kama zana ya kujikuta na kujiponya kutoka kwa uzoefu wa maisha, changamoto, shida za zamani na zinazoendelea.

## Kwa maoni yako ni athari gani tunatarajia kujitokeza wakati huu wa janga kubwa?

Mchoro huu unahusu mada ambazo zinazingatiwa na eneo la sanaa ya kisasa kuwa rahisi, lakini kutoka kwa mtazamo wangu ni muhimu; urafiki, upendo, uunganisho na ushirika. Vipande vilivyochaguliwa hushughulikia hisia tofauti kama kutengwa, upweke na mali. Ninaamini kuwa wakati wa janga hili la sasa la COVID - 19, wanadamu wote wanafahamu umuhimu wa maadili na hisia hizi rahisi, kutulazimisha kuunda aina mpya na njia za mawasiliano.
Wakati ninapofikiria juu ya hali ya sasa na jukumu la sanaa na athari zake maswali mengi huja akilini mwangu kuhusiana na ajenda za sanaa na umuhimu wake kama kifaa cha kuonyesha sauti za wale ambao hawafurahii haki za kijamii na kisiasa, na ukweli wa mawasiliano na kushirikiana kati ya wasanii. Na licha ya mashaka na maswali yote, sanaa inabaki kuwa wokovu wa kweli kwa usalama wa mwili na kiakili. Sanaa inatupatia Nafasi ya kupata Wokovu Kamili na Usalama.



Hii kuma imekuwa ikivuja mateso kwa muda mrefu sana kwangu kukumbuka,
Yule ajuza anasema akivizia makusudi katikati ya miguu yake
Sana zaidi, ikijaribu sana hadi ikawa kawaida, hadi kati ya mfupa ndani
Ninajaribu kukaa kutulia ndani yangu binafsi katika hali yangu ya kukosa utulivu
Anasonga na upepo wa ukweli chini zaidi ndani ya ardhi anayoikalia
Siku hizi, sauti ya ouma ni ya kutuliza kwa kujua, kutuliza wasiwasi wa ndani,
kana kwamba ni moja na ukimya unaozunguka angani.
Na bado nilijua bila shaka, wakati nikiita - Dada! Dada! -
Wangekuja kwa kasi ili kunibeba kunipeleka nyumbani
Mwili huu, mweusi. Umechanwa vipande vipande kwa muda mrefu,

Kaa kimya usimwambie mtu yeyote, italeta aibu kwa familia yetu, walisema

Upweke mwingi,
mno kukupelekea wazimu, kwa hivyo wakati walisema shida, nilijua kwa nafsi yangu yote jinsi inavyoonekana, niliionja, ni liihisi. Ninaiishi.

## Hili si Jambo Geni Kwetu

## Na: Irene //Garoës, Namibia

Kuma za wanawake Waafrika zimekuwa zikivuja damu mateso kwa muda mrefu zaidi sana
kujaribu kuwa ya kawaida hadi
kati ya mfupa wa ndani

Na bado anajua bila shaka yoyote kuwa wakati anapoita
Dada! Dada!
Wanakuja kwa kasi, kila wakati bila shaka

Miili hiyo myeusi ya wanawake wa Kiafrika imevurugwa vipande vipande kwa muda mrefu sana
Kaa Kimya (usimwambie mtu yeyote, italeta aibu kwa familia yetu, walisema)
Upweke chungu nzima
Sana kunitia wazimu

Na bado bila swali walifika na kukaa naye mchana na usiku, wakikumbuka haswa jinsi ilivyohisi, wakiijua, wakimujenga te na upya, tofali baada ya tofali.

Sauti za wanawake wa Kiafrika zimegandamizwa kuwa kimya kwa muda mrefu sana
Kelele nyingi sana (walisema)
Kwa hivyo walijaribu kumnyang'anya yale yote aliyoyajua
**Wanaendelea tu kuchukua na kuchukua wanaendelea tu kuchukua na**
**kuchukua akili, mfupa, ngozi, damu, Mungu - na bado, hakupoteza chochote.**
Maana walipomsikia akilia Dada! Dada!
Walipiga kelele kutoka kwa undani wa tumbo lao kwa uchungu, bila kuiruhusu kuingia, walipiga mayowe na kumshikilia k wa nguvu wakati wote wa siku za giza ya ngurumo za radi

Kwa hivyo sasa, ukimya ukiwa unazingira ulimwengu na tumefungiwa kizimbani pamoja na wanyama halisi, kufunikwa kati ka kile kinachodaiwa kuwa kiama cha uoga ila kujua hapa sipo mahali ambapo ndoto zetu zinakuja kuangamia, hili hapa hivi silo jambo geni kwetu!

Wanawake wa Afrika hawajasahau kuwa nguvu zao ziko miongoni mwao
Walikaa pamoja
Waliimba pamoja
Walikula pamoja
Wakapashana joto pamoja
Na walijua kuwa ilikuwa wakati wa mama ulimwengu kuponywa

Na watu walielewa hii kwani anadai mali ambayo ni haki yake, anaendelea kuwa shujaa, hadi tu ndoto zake zinaweza ku mchukua bega kwa bega pamoja na za dada zake, watu wake.
Yeye alijua, wao walijua kuwa kila kitu tulichodhani tumepoteza kinapatikana tu ndani yetu.
Wanawake wa bara hili wanainuka, wanvuja damu ya mapenzi, wanazaa uhuru, ili waweze kuwa.
Kutambua kwamba sisi, Wanawake wa Afrika tunvuaj damu ya maisha iwe dhahiri.


# USAANI KWA UPONYAJI

**Feminist Republik (FR) ilipatana na Anne Mwiti (AM), msanii wa Kenya, mtafiti, msanii wa Citizen Ulimwenguni Awardee 2014 na mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kenyatta nchini Kenya ili kujadili juu ya umuhimu wa sanaa na ubunifu kwa ustawi, uponyaji, uzuri, mawasiliano na kuweza kupitia shida.**

**Tumejua kuwa sanaa na ubunifu ni muhimu sana kwa ustawi, tiba na uponyaji kwa sababu uzuri una jukumu katika maisha yetu. Je! Sanaa yako imeathirije maisha ya wanawake na watu wengine?**

AM: Kuwa msanii mkubwa kunamaanisha kuishi karibu na hisia zako iwezekanavyo ili uweze kutoa kitu ambacho ni cha kipekee kabisa. Sanaa yangu imekuwa ikiboreka kwa muda na kwa kila awamu nimeona ikibadilisha jinsi watu kwa ujumla wanachukulia wasanii wanawake na haswa jinsi wanawake wanavyojiona katika kazi inayotawaliwa na wanaume. Imewahimiza na kuwahamasisha wanawake wengine kuwa wasanii. Sanaa ni aina ya mawasiliano sio tu kwa msanii anayetengeneza hiyo sanaa bali kwa watumiaji pia. Sanaa yangu imekuwa sauti kwa wale ambao hawawezi kusema juu ya maswala ambayo sanaa tu ndiyo inaweza kuelezea vizuri.







**Tunapojaribu kujizatiti na kujikakamua kustawi katika msimu huu wa COVID - 19, tungependa kusikia kutoka kwako jinsi ambavyo kazi yako inaleta taswira inayohusu hadithi ya jinsi tunavyosafiri safari hii.**

**AM**: Nimefurahia sana kazi yangu. Ni mawasiliano kutoka kwa akili yangu, moyo, roho kupitia mikono yangu kama tafsiri ya hali ya kihemko katika kile kinachoendelea kakita mazingira yangu. Ni njia yangu ya kupata sauti ambayo inaelezea hisia zangu za ndani, ndoto zangu, lugha yangu na msamiati wa mawasiliano ya kitu ambacho mimi huona kuwa muhimu. Kwangu mimi, COVID-19 ni baraka inayoonekana kama siyo. Mimi ni mwanamke aliye na ajira na familia na kupata masaa marefu ya nafasi ya ubunifu isiyoingiliwa ni vigumu sana. Hiki kimekuwa ni kipindi cha muda mrefu kwangu ambao hufanya siku kuhisi kama zawadi ya kuwa na wakati ambao haujajazwa chochote. Ninaufurahia. Nimepata fursa ya kufanya kazi kwa masaa mengi bila kuangalia kile ninachofanya hadi kazi imefikia hatua ambapo ninajua ni nini ninahisi . Walakini, kama msanii, nimeangalia hadithi yangu ya taswira kuhusu COVID-19 ikibadilika kutoka kwa virusi vyenyewe na athari zake kwa ubinadamu kuishinda na mwishowe hadi kufikia kutafakari siku zijazo na tumaini kubwa na uelewa wa njia za kubadilisha athari zake.

"Imekuwa wakati mgumu sana kwa watu wengi wakati wa kusitishwa kwa shughuli muhimu ila kutazama kazi mpya za sanaa ambazo ni za kufaa sana kwa kile wanachokipitia kumefanya kipindi hiki kuonekana kama sisi sote ni jamii moja yenye matatizo sawa..."

# Usaani kwa uponyaji



**Kama mtu anayetoka miongoni mwa wataalamu wa kimasomo au chuo kikuu, je kazi yako inawahusu vipi wanawake kutoka ngazi zote za maisha? Wanawake wasio wasomi wapataje uhamasiho na hii sanaa yako yenye nguvu?**


Kufanikiwa katika sanaa sio tu kujulikana na kuuza sanaa lakini pia kwa jinsi watu wanaona kazi yako na wanahusiana nayo.

Ulimwengu wa wasomi ni nafasi tofauti sana ambayo haihusiani na nafasi ya sanaa katika kujieleza na uwasilishaji. Njia moja inayojulikana ambayo wanawake wameamua kujihusisha na sanaa yangu ni kutambua jinsi sanaa yangu inavyochochea mhemko kwao na kuonekana kuhusiana nao kwa kiwango cha kibinafsi. Wanawake ni turubai ambayo kwao tunaweka hisia zetu, zile nzuri na mbaya. Na, mimi mwenyewe kama mwanamke, naona na nanahisi na wanawake na kuelezea hofu mbaya zaidi walizo nazo kuhusu watoto wao katika sanaa yangu; upendo wao na chuki zao na hata wasiwasi wao wa kutojuwa ya kesho.



**Kuna fursa zipi zinazopatikana za kuungana kikamilifu na kila mmoja, huku tukifanya kusudi la kuweka sanaa na kujieleza kwa ubunifu kama njia ya matibabu na uponyaji haki?**

AM: Ni machache sana yameandikwa juu ya mabadiliko ya wanawake kutoka kwa kuhusika katika familia hadi kujaribu kujipatia uhuru. Ni vigumu sana kustahimili hayo kwa sababu hisia nyingi huingia katika kile unachofanya wewe kama mwanamke katika mambo haya yote ya maisha kama vile mwanamke aliyeajiriwa mwenye taaluma, kutoa msaada wa nasaha kwa familia wakati mtu anafuatilia mandhari ya uumbaji wa sanaa. Ni muhimu kuunda mitandao inayounganisha wanawake na kuwafungulia fursa kwao kwa kuandamanisha ubunifu wao kuwa mapato ya kifedha.


MWITI
2020

# Usitie Shaka!

Kufumba na kufumbua jicho; kama miale ya dhoruba
Kuchanganyikiwa, wasiwasi, uwoga, upweke, kukata tamaa
Ulimwengu ulivamiwa ghafla, kama vile wingu jeusi lenye uovu
Mkurupuko ukaachiliwa; Kuongezeka upesi kuwa ambo
Corona Virus ndo jina lake; COVID-19; jina la kitani
Ulimwengu ukatulia kimya; kulemazwa hadi kupiga magoti
Kuathiri na kuambukiza; kung'oa maisha kutoka kila pembe
Penye shida tunapata ujasiri wa kupanga, kujikusanya, kupambana
Ndisi sisi mwanga wa tumaini - Nuru ya mionzi
Hatutajisalimisha kamwe; hatushindwi katu; ushindi tu,
Usitie shaka; hili pia litapita

Misemo ya kutoa matumaini; istilahi isiyosahaulika
#Kusitishwa katikhuli 2020, #kujitenga-binafsi, #karantini
Misemo ya kuanza upya, desturi zilizosahaulika muda mrefu
#Nawa mikono mara kwa mara; #jamii kukaa kutokaribiana
#adabu za kukohoa; uangalifu - ni sharti
Fikra na tafakari; mabadiliko yaliyo chanya
Mataifa yetu yanatoa kauli; kubadilika ili kupata maendeleo
Misemo ya kuokoa; misemo ya tahadhari
#Kaa nyumbani #kaa salama, #zuia kuenea
Ratibu, shirikiana; jitume katika kutoa huduma
Giza la usiku huenda ni refu lakini lazima hatimaye hakika kutakucha
Usitie shaka! hili pita litapita

Huku tumezama katika kuthubutu kutumaini - ni kupata ushindi
Ujasiri kukumbana na shida - ushindi ndio dhamira yetu
Kwenye mwanga wenye imara - siku mpya inazaliwa
Katika moyo wa kujitolea kudhahibu – ubinadamu unadhihirika
Kujituma kuokoa hata penye tishio la kifo
Ndiyo kauli mbiu ya mhudumu wa afya
Kwa mshikamano, umoja; COVID-19 hatimaye itashindwa
Mkae wenye utulivu ila pia ufahamu; mjihami na taarifa za kuaminika
Barabara inaonekana ndefu yenye matata mengi lakini ina mwisho
Kamwe! msitie shaka! hili pia litapita

**Na Bernadette French, Sierra Leone**

# "Upinzani Haujafutwa"

Kama sehemu ya Uangaziaji wa Mshirika, Feminist Republik (FR) walipatana na Mwanaharakati wa Kifeministi mwenye Jinsia Tata na Asiyeaja Jina, almaarufu Anonymous Queer Feminist (AQF) anayeishi katika nchi za Misri na Sudani kushiriki maoni yao juu ya upinzani, kuandaa na kufanya kazi inayohusu masuala kadhaa yaliyoshindaniwa kama vile za Walio Wachache Kujamiiana na Kijinsia (haswa masuala ya SOGIE na Kazi ya Ngono huko Afrika Kaskazini - huko Misri na Sudani). Mahojiano yaliangazia muktadha wa kufanyia kazi, changamoto zinazowakabili, jinsi wanaharakati wanaweka vichwa vyao juu ya maji, uvumilivu unaonekanaje kwao na fursa zilizopo za ushirika na WHRD wengine wa Kiafrika kote Barani. Hapa chini ni vielelezo vya hayo mahojiano:

**Tunachukua muda wa kuomboleza na kutoa heshima zetu kwa mwanaharakati wa Kimisri Sarah Hegazi**

## 1. Je, ni changamoto gani unazopitia katika muktadha wako ambazo hupunguza haki na uhuru wako?

Kwa upande wa sheria na sera, Sudani na Misiri zote zina sheria zinazorudisha nyuma ambazo zinaongeza kutengwa na ukiukaji wa haki za walio wachache kujamiiana na kijinsia. Kwa mfano; Wamisri wanashtaki watu wa LGBTIQ + licha ya kukosekana kwa amri ya kisheria iliyo wazi ambayo hutoa vifungu vya kuharamisha uhusiano wa jinsia moja na; baada ya kukamatwa kwa kesi, Sheria 10/1961 kuhusu Kukumbana na Ukahaba ndiyo mara nyingi hutumika. Kufuatia hilo; kuna idadi inayoongezeka ya watu wanaokamatwa na kushtakiwa kila mwaka katika kesi za usherati ambazo zimeongezeka mara tano na wastani wa watu 66 kwa mwaka. Kwa wakati huo huo nchini Sudani, mfumo wa mahakama unatekelezea Sheria ya Kiislamu ya Sharia na vifungu vya 148, 151,152 vya Sheria ya Jinai yaani Penal Code ya Sudan inaharamisha kitendo cha 'ushoga' (ngono ya mkunduni iwe baina ya wanaume na wanaume au hata na wanawake).

Kwa kuongezea, shughuli za Asasi zisizo za Kiserikali nchini Misri zimedhibitiwa na Sheria 149/2019 sheria ambayo inazuia uhuru wa kujumuika na kukusanyika kwa asasi za raia ikiwa ni pamoja na vikundi na mashirika yanayofanya kazi kwenye masuala ya SOGIE na inatoa nafasi ya ukiukwaji zaidi, udhalilishaji na vitisho dhidi ya watetezi wa haki za binadamu na vikwazo vingi vya ufadhili. Kuongeza kwa hili, kuwa mwanaharakati na sehemu ya shirika la LGBTI mara nyingi hufikiriwa kama suala la usalama wa kitaifa na katika visa vingine sheria za kupambana na ugaidi zimetumika kuwasaka wanachama wa makundi na mashirika yanayofanya kazi ya SOGIE. Katika visa vingine, Sheria 175/2018. Sheria ya Kupambana na Ujangili wa Mitandaoni imekosolewa kwa kutumiwa kukuza uzuiaji uhamishaji, utunzaji wa data na uchunguzi na madai ya "usafirishaji wa data kati ya serikali zingine.'

Ulinzi na usalama wa kiwmili na Kidijitali unabaki kuwa changamoto kubwa kwa watetezi wa haki za binadamu wanaotetea haki za watu wa LGBTI huko Afrika Kaskazini.
Kuzingatia sheria zilizotajwa hapo awali, kama mwanaharakati wa LGBTI, ninakabiliwa na changamoto katika kudumisha ulinzi na usalama wangu.

Kama mtu wa ujinsia tatnishi anayeishi katika mazingira ya uhasama wa kimfumodume ambayo yanakuza chuki, kutengwa, kutokubalika na uchochezi dhidi ya watu wa LGBTI.

Hali ya kisiasa na kiuchumi inachukua jukumu kubwa katika utulivu wa kazi ya umma, sekta ya kibinafsi na kazi za Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Demokrasia dhaifu, vita na migogoro na hali mbaya ya kisiasa na mfumko mkubwa wa uchumi inawakilisha changamoto kubwa kwa miradi na huduma zinazotolewa na mashirika ya asasi za kiraia. Huu ni ukweli hususan katika nchi ambazo zimepata mageuzi na mapinduzi ya mara kwa mara ya kijeshi, kama vile Misri na Sudani.

Mwishowe, kama sisi sote tunavyojua kufikia hivi sasa, nchi zetu nyingi zimeanzisha mifumo ya Kupambana na COVID-19 ambayo baadhi ya mifumo hiyo imefanikiwa ila mingine imekuwa na athari hasi kwa baadhi ya sehemu za jamii hususani kwa wale walio wachache kwa kujamiiana na kijinsia. Kwa hivyo hii inafanya janga la Afya na COVID-19 kuwa moja ya changamoto tunazokabili kwa sasa. Kama njia ya kudhibiti mgogoro huo, Serikali ya Misri inaendelea kutumia sheria za hali ya dharura na hivi karibuni iliidhinisha fungu la marekebisho yaliyopendekezwa kwa Sheria ya Dharura ya Misri ambayo athari yake kuu ilikuwa ni kuongezwa kwa nguvu na uwezo wa urais. Wakati Misiri ikiendelea kutekeleza sera za wananchi kufanya kazi wakiwa nyumbani kwao, kufunga kwa asubuhi kwa maduka makubwa, vituo vya ununuzi na mikahawa, nafasi za umma, sekta za kibinafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali; hali inayoendelea ya kuzuiliwa kwa shughuli zozote wakati wa usiku huathiri vibaya wale walio kwenye pindo la jamii - mahali watu wa LGBTI wanapatikana. Vile vile, huko Sudani, sheria kali ya kusitishwa kabisa kwa shughuli kwa masaa 24 inaingia mwezi wa pili na imechangia kupooza kabisa kwa hali zote za maisha. Hii inaathiri vibaya hali ya kisaikolojia ya wanaharakati na jamii za LGBTI haswa wale ambao walijikuta wamefungwa na wanaowadhulumu (familia au wenzi wao). Kwa kuongezea, ukweli kwamba sekta nyingi ambazo zimefungwa ni zile ambazo watu wa LGBTI wanapatikana huathiri ustawi wao wakiuchumi, adhi na riziki yao.

**"Ninakabiliwa na unyanyapaa mwingi wa kijamii na ubaguzi. Kwa hivyo, kupata usawa kati ya usalama wangu wa kibinafsi na kuwa mwanaharakati wa LGBTI ni changamoto nyingine...."**

# 'Upinzani Haujafutwa'

## 2. Wakati wa hofu, machafuko na wasiwasi; nini kinawasaidia kuweza kuendelea kama wanaharakati wa LGBTI, kama Asasi na Ushirikiano?

Kutunza ustawi wangu, kama mtu binafsi ni muhimu sana wakati wa shida. Kwa kuongezea, kutunza afya ya kisaikolojia ya kila mmoja, ni muhimu sana kwa tija ya kikundi. Sisi kila wakati tunahakikisha kwamba hakuna kazi kubwa zaidi kwa mtu mmoja ila husambaza kazi hizo miongoni mwetu sisi sote, na hakuna lawama kwa watu ambao wanaelezea kutofaulu kwao kuhimili shinikizo, hatari na wasiwasi ambao unakuja na kufanya kazi kwa muktadha wa hali ngumu na maswala yaliyogombewa sana ya siasa za mwili na kujiamulia. Tunaheshimu pia kwamba wakati mwingine wengine wetu wanahitaji wakati wa kupumzika na kujifanya wapya. Na bila shaka; mawasiliano madhubuti kama ya pamoja na kuelezea shukrani zetu kwa kila mmoja hutumika mara kwa mara kwa kuhakikiana na kuhimiza uwezo wetu wa kupinga na kupambana.

## 3. Je! Kuna mipango yoyote kadhaa ambayo inazingatia ustawi na utunzaji usiokuwa wa kawaida tu?

Sijui iwapo kuna mipango ya Misri na Sudani ambayo inazingatia ustawi na utunzaji pekee, lakini katika miaka michache iliyopita mashirika mengi yaligundua umuhimu wa ustawi. Pia, mashirika na vikundi vingine vya LGBTI viliunda miradi ambayo hutoa huduma za usaidizi wa kisaikolojia bure au miradi inayo zingatia matibabu ya kisanaa

## 4. Tafadhali shiriki mifano kadhaa ya njia unavyojitunza kama wanaharakati.

Kuna njia anuwai ambazo tunajitunza ambazo ni pamoja na: Kufanya mazoezi ya kutafakari na yoga; Tiba ya sanaa ambayo ni pamoja na kucheza, kuchora na kuchonga; Mazoezi ya mwili ikiwa ni pamoja na kutembea na kunyoosha viungo; Kusikiza muziki; Kujitengea wakati wa kupumzika; Kuzungukwa na watu wenye kupenda, wenye kujali (familia, wanaharakati wenzako na marafiki wa karibu) na; Kutafuta msaada wa wataalamu (mwanasaikolojia/ mtaalamu wa akili) kama inavyotakiwa na inapohitajika.

## 5. Nini maana ya ustahimilivu katika Harakati za Misiri na Sudani?

Licha ya vurugu za kijamii, sheria za kibaguzi na kubanwa kwa nafasi, wanaharakati wa LGBTI katika nchini Misri na Sudani wanaweza kutafuta njia mbadala na za ubunifu kwa harakati zao kama: sanaa, afya na michezo, kwa kutumia urafiki mtandaoni na majukwaa ya media ya kijamii kuleta kujulikana kwa maswala yao , kujenga ushirikiano na umoja kupitia njia ya kuingiliana. Kuongeza kwa hii, harakati hapa zinachukua hatua za ulinzi na usalama kama kipaumbele katika nyanja zote za kazi zao.

## 6. Ni fursa zipi za kuungana kwa kina sana na Wanawake Watetezi wengine wa Haki za Binadamu wa Afrika ambao husisitiza ustawi kwa njia ambazo zina msingi wa haki, makutano na muungano Afrika?

Linapokuja suala la nafasi za mwili, kwa sasa kuna fursa chache za kukutana na Watetezi wengine wa Haki za Binadamu wa Afrika ambao hutumia njia zinazohusiana, haki na msingi wa haki ya uponyaji. Walakini, kuchukua fursa ya teknolojia na nafasi za mkondoni, kushiriki hadithi zetu za mapambano ya kila siku kupitia njia za kutazama-sauti na kulenga mikakati ya uponyaji na ustawi, tutaunda mshikamano na uhusiano kati yetu na WHRD wengine wa Kiafrika.

# Dzuwa - Maswali ya Jaribio

NA ZANELE MBUGUA

Tungependa kusikia kutoka kwako! Dzuwa ni nini bila kusikia kutoka kwako! Je! Ulijua jina letu Dzuwa ni neno la Kichewa la 'kuchomoza jua'? Je! Unaweza kutuachia barua pepe (tazama hapa chini) na tujulishe neno unalotumia la 'kuchomoza jua' na tutayachapisha haya kwenye matoleo ya baadaye. Wacha tuufanye mchakato wa kujifunza na kuunganisha kuwa wa kufurahisha kwa kuongeza utamu wa viungo! Tuma majibu yako na tutataja washindi 5 wa kwanza kwenye toleo letu linalofuata!

## Ukweli wa Kufurahisha:

Je, ulifahamu kuhusu Ziwa la Pinki nchini Senegal?? Linapatikana kaskazini mwa peninsula ya Cape Vert nchini Senegal. Linajulikana pia kama **Mto wa Retba**, hili bwawa ambalo halina urefu wa kina na limezingirwa na matuta ya mchanga na ni mahali amabapo panawavutia sana kwa ziara za mchana wenyeji wa jiji kuu la Dakar almaarufu dakarois na hata pia watalii, wote wakitaka kufurahia utulivu wa ziwa hili na kiini macho cha uganga wa bwawa hilo – muonekano wa rangi nzuri ya pinki ambayo wakati mwengine huonekana kuibadilisha rangi ya maji yake. Taswira hii ya rangi ya pinki husababishwa na ile hali ya kuwepo idadi ya juu sana ya chumvi ambayo ni zaidi ya mara kumi ile inayopatikana kwenye maji ya bahari. Ni eneo lenye urembo wa kipekee ambao unaweza kufurahiwa mwangaza ukiwa sawa kabisa – nafasi nzuri zaidi kuweza kuyaona maajabu haya ni katika msimu usio na mvua na kuwasili pale jua likiwa liko juu.

## Jibu Maswali!

**Swali la 1:**

Watetezi wangapi wa Afrika wa WHRD walikutana kwenye kongamano la jijini Abuja, Nigeria ili kujadili mtiririko wa mawazo na kushauriana ili kukubaliano iwapo jukwaa la Feminist Republik linahitajika?

**Swali la 2:**

Ni mbinu gani ya pili ya uponyaji inayotumiwa na mponyaji Fatime Faye?

**Swali la 3:**

Ni lini na wapi ndipo uanzilishi wa tamasha ya Feminist Republik uliandaliwa?

**Swali la 4:**

Taja mbili baina ya mbinu za kujitunza kibinafsi ambazo yule anayejiita "Anonymous Queer Feminist Activist' alishiriki ya kuhusu utunzaji wa kibinafsi na utunzaji wa pamoja?

**Swali la 5:**

Je, Liz Ombati alikuwa macho saa ngapi?

Tutumie majibu yako sahihi pamoja na jina lako, nchi, unachofanya hivi sasa na njia mbili unazozipenda za kujitunza mwenyewe binafsi na jamii yako? Peperusha majibu yako na habari kwa feministrepublik@uaf-africa.org

# Utambulisho wa Waliochangia



Amal Hamed (أمل حامد): Mbuni wa picha na mchoraji kutoka Cairo, Misri, ambaye anafanya kazi katika uwanja wa haki za binadamu na wanawake. Mhitimu kutoka Chuo Kikuu cha Cairo, Idara ya Falsafa (2011), Amal alishiriki katika miradi kadhaa inayohusiana na wafungwa wa dhamiri, almaarufu Prisoner of Conscience, nchini Misri na Chama cha Uhuru cha Kufikiriana Kujieleza (AFTE - Association for Freedom of Thought and Expression). Alishirikiana na wasanii wengine kutoka nchi tofauti kwenye mradi ulioandaliwa na asasi ya Take Back the Tech (Mexico) akilenga kueneza ujumbe mzuri wa mshikamano kwenye wavuti kupitia uchoraji wa wanawake. Amal pia alishiriki katika miradi kadhaa na masomo ya kijinsia ya Ikhtyar Gender Studies Research Space ikiwa ni pamoja na,"Kuwa Mtandaoni kama Mfeministi" na "Kuunda Wavuti wa Kifeministi". (Unaweza kupata Amal kwenye Instagram(@amalartworks na Behance



Anne Mwiti ni msanii wa Kenya na mtafiti. Yeye yuko katika hatua za mwanzo za kuifuatilia shahada yake ya Uzanifu au PhD kuhusu mada: Mgogoro, Ugomvi na Utamaduni: Jukumu la Sanaa. Yeye hufundisha sanaa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Yeye ni msanii aliyefanikiwa kuonyesha kazi yakemiaka mingi sasa.
Email: annemwiti@gmail.com
website:www.saatchiart.com/annemwiti



Anonymous Queer Feminist amekuwa mwanaharakati kwa miaka mingi katika masuala ya mwelekeo wa kijinsia na utambulisho wa kijinsia huko Misri na Sudani.



Bernadette Abioseh French ni mtetezi mashuhuri wa haki za binadamu mwenye nguvu na mchambuzi wa masuala ya kijinsia, na ana uzoefu wa utetezi wa miaka 14 katika haki za binadamu, haki ya mpito, Jinsia, Haki za wanawake na ulinzi wa watoto, ambaye kimsingi amejituma kwa kutetea upitishaji wa sera, utoaji wa mifumo madhubuti ya majibu pia ameongezea ari ya ufukiaji wa kuzuia na kulinda wanawake na wasichana kutokana na kila aina ya dhuluma za kijinsia na Ujinsia. Amepevuka sana na kushamiri katika ulingo wa kutunga mashairi kama njia yake ya kusimulia uzoefu wa wanawake wa unyanyasaji wa kingono na kijinsia.

# Utambulisho wa Waliochangia



Cynthia Happi ni raia wa nchi ya Kamerun anayeishi na kufanya kazi nchini Uhabeshi as a Mtafiti wa Masuala ya Amani na Ulinzi. Cynthia ni mpenda muziki ambaye ana shauku kama shabiki wa soka. Unaweza kumpata Cynthia kwenye Instagram: @cynthiahappi



eloise burke: Asili yangu kama Mwafrika mkimbizi ila makazi mseto wa Afrika, Karibian na Kanada imenipa uzoefu wa anuwai, mali, hila zilizo na habari, na ujuzi wa hali ya juu ambao ni wa kipekee kwa kushawishi njia yangu. Vyombo hivi vimekuwa vikijenga mashirika kwa undani na kwa nguvu kwa zaidi ya miaka thelathini. Kwa mazowea, ninaposhiriki kuunda shirika na kasha nikatoka, sijawahi kwenda kabisa…
Email: eloiseodp@gmail.com
LinkedIn: eloise e. burke



Fatime K. Faye alizaliwa mnamo 1957 huko Dakar, Sénégal. Baada ya kuhitimu na shahada ya BA katika lugha ya Kiingereza kutoka Chuo Kikuu cha Dakar, alifanya kazi kwa miaka kadhaa na Ubalozi wa Amerika huko Senegal. Alihama mnamo 1987 na kuelekea huko Guinea Conakry kwa miaka 2 ambapo alianza kufanya kazi bila mwajiri maalum. Mnamo 1989 alirudi Senegal ambapo alifanya kazi kama mwandalizi wa mawarsha na mikutano ya mashirika ya kimataifa. Kwa sasa anaishi Toubab Dialaw (umbali wa kilomita 60 kutoka Dakar) katika kijiji kidogo cha uvuvi ambapo anafanya kazi kwa ukarimu na vyama vya wanawake na vile vya vijana. Pamoja na shughuli zake za kitaalam, mara nyingi alijihusisha na vyama vya vijana haswa katika masuala ya michezo na utamaduni, uundaji wa biashara za wanawake na afya. Yeye ni mwanachama wa Chama cha Maendeleo Jumuishi huko Toubab Dialaw, Vilabu vya Kimataifa vya Toastmasters na Mtandao wa Afrika wa Viongozi almaarufu Pan African Network of Leaders - (PANeL).



Françoise Moudouthe ni mfeministi wa muungano wa Afrika na mwanzilishi wa asasi ya Eyala, jukwaa linalotumia lugha mbili Ili kuhamasisha nguvu za mazungumzo Ili kuchanganua maana ya kuwa mfeministi Mwafrika enzi hii.

Unaweza kuwasiliana na Françoise kupitia: www.eyala.blog/ @EyalaBlog kwenye Twitter & Instagram

# Utambulisho wa Waliochangia



Irene //Garoës ni Mfeministi na Mhamasishaji wa Jamii kutoka kwa kijiji kidogo kiitwacho Leonardville katika sehemu ya mashariki ya Namibia. Amejitolea kuendesha ujenzi wa harakati za wanawake kwenye ngazi ya vijijini na vikundi vya wanawake walioeletengwa nchini Namibia. Yeye hufanya kazi na mashirika ya haki za wanawake (wanawake asilia, wanawake ambao wanaishi chini ya sheria za kitamaduni, wasagaji, na wanawake wa vijijini) na hufundisha vijana juu ya maswala ya haki za binadamu, Haki za Kijinsia na Kiuzazi, utatuzi wa migogoro na uponyaji kutoka kwa vurugu kutumia njia mbadala, vile vile kuandaa na kuratibu ukufunzi na mafunzo ya ustadi wa maisha na viongozi wa dini, kuwapa mafunzo wanawake wa umri mdogo katika kujilinda, maonyesho ya sarakasi na kuigiza, uandishi, uongozi wa kifeministi na ujengaji wa harakati. Irene anafurahia ushairi, kusimulia hadithi, maandalizi ya filamu na anapenda kujua tamaduni za wengine tofauti, mbwa na bustani. Irene pia ni Mratibu wa Nchi katika asasi ya One Billion Rising Namibia na ana Shahada ya Mawasiliano (Honours) kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Namibia (NUST).



Joia Sabimana Mimi ni mwanamke kutoka nchi ya Burundi mwenye umri wa miaka 28. Mimi hujitambulisha kama queer – na nimefanya kazi ya utetezi katika mashirika ya nchini ya LGBT+. Nimehitimu masomo ya Saikolojia, lakini nimeweza kukuza shauku ya dhati ya uandishi. Mada ya mara kwa mara kwenye mashairi yangu ni uhuru kutokana na kukandamizwa na uzoefu wa msichana wa Kiafrika akijaribu kuupata mkondo wake kwenye bahari ya mifumo ya dhana za kijamii ambayo anajipata katikati yake. Msisitizo huu unatokana na uelewa ya kwamba uzoefu wa kike una haja ya kusimuliwa. Mimi hujizuia ninapopata fikra ya kuingia kwa kina sana maswala ya shauku ya pamoja ya kike, kwa sababu ya kuogopa yale maumivu ambayo inaweza kuamsha. Lakini kina kama hicho kinahitajika iwapo uponyaji unatakikana kutokea. Ukumbatiaji wa shauku ya kike iliyo ndani kwa kina huambatana moja kwa moja na kusikiza mwito wa itifaki ya mhusika kuweka imani kwa uelewa wa mtu wa moyoni, na kujikubalia mwenyewekuishi kwenye maeneo ya uhatarishi. Hivi ni vito muhimu vya kike ambavyo aghalabu hupotea katika vita vya kutaka kuishi. Mwishowe, natumaini ya kwamba nitaifunua pazia inayoficha uzoefu wangu katika juhudi ya kuwatia moyo dada zangu ili nao wasiogope kufanya vivyo hivyo.



Liz Ombati: Mtetezi wa haki za walemavu ambaye hujitetea binafsi. Utetezi wangu unakuja kupitia uzoefu wangu wa kuishi na hali ya ulemavu wa afya ya akili. Nilianza kuandika tangu umri mdogo sana, kwani ilikuwa njia bora kabisa ambayo ningeweza kuelezea kile kilichobaki bila kusemwa. Kuandika kwangu ni aina ya tiba. Ninatumia kuandika kutuliza mabadiliko; kuteka usikivu juu ya ukandamizaji, na kuzingatia tahadhari kwa dhuluma zinazonizunguka mimi. Ninaandika juu ya hasira iliyo ndani yangu na kufadhaika kwa kutoweza kuifanya dunia kuwa bora kwa kila mtu. Ninaandika ili kujikuta nafsi yangu kila ninapojikuta kwenye uchungu mwingi na dhiki kwa sababu ya ndoto zisizotimia. Walakini, ninaandika pia kuelezea uzuri na matumaini yanayonizingira. Ya sasa, ambayo ni matokeo ya miaka mingi ya jana. Ninaandika kuhusu upendo na hamu; juu ya kuipata nafsi yangu mwenyewe; juu ya uponyaji. Ninaandika juu ya matamasha mapya na matumaini mapya. Kuhusu kutoka kwa jua na kutua kwa jua. Ninaandika kuhusu ile ahadi ya ulimwengu wenye usawa. Dunia iliyo salama kwa sisi sote. Ulimwengu ambao unatutosha sisi sote; kushiriki katika mshangao wake na uzuri. (Barua pepe: lizombati@hotmail.com
Blog https://elizabethombati.wordpress.com



Masa Amir ameajiriwa na shirika la UAF-Africa kama Mratibu wa Utafiti na Ulinzi wa shirika hili. Maza ana uzoefu katika kukusanya na kuhifadhi nyaraka zinazohusu dhuluma walizopitia Wanawake Watetezi wa Haki za Kibinadamu (WHRD)na kuendesha utetezi katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa almaarufu Human Rights Council na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu – almaarufu African Commission for Human and Peoples' Rights. Anaegemea sana masuala ya haki za kiuchumi za wanawake na uimarishaji wa taratibu za ulinzi na usaidizi kwa WHRD walio hatarini, huku akilenga sana wale EHRD walio katika maeneo ya Afrika ya Kaskazini. Masa alihitimu na shahada ya Uzamili, yaani Master's Degree katika somo la Sheria za Kimataifa za Haki za Binadamu kutoka katika chuo kikuu cha American University in Egypt, nadharia yake ilizingatia haswa jinsi ambavyo ukiukwaji wa haki ya ulinzi wa kijamii unachangia umaskini miongoni mwa wanawake nchini Misri.

# *Utambulisho wa Waliochangia*



Nancy Chela Cherwok alizaliwa jijini Nairobi, Kenya mnamo 1992. Yeye hufanya kazi kimsingi ya uchoraji kutumia rangi; kutumia akriliki kwenye turubai na karatasi. Alisomea Uundaji na mifano katika mchoro. Mada kuu ambayo yeye hushughulikia iko kwenye tamaduni na utambulisho. Yeye hufanya matumizi ya alama, rangi na miundo kuongezea muundo kwenye kila kazi yake ya uchoraji. Mwezeshaji huko Grafitti Girls Kenya, warsha inayotumika kuwashirikisha kuwashirikisha wasichana kwenye grafiti kama mfumo wa sanaa ambapo wanajadili, kushiriki na kushirikiana kwenye miradi wakiweka msisitizo katika uhamishaji wa stadi. Mbuni wa michoro ya kwenye kuta na mfungaji katika tamasha ya Koch Fest inayoandaliwa chini ya asasi ya Dada's Connect ili kuhamasisha wasichana na wanawake wa unri mdogo kwa kutumia vipande hivyo vya sanaa. Instagram: https://www.instagram.com/chelwek/ and Behance: https://www.behance.net/NANEY_CHElACHELWEK



Raquel Lima ni malenga anayeishi Lisbon mwenye asili yake mchanganyiko - ikiwemo kingo zote mbili za Mto Tagus na Bahari ya Atlantic: kuanzia kwa mamake aliyetoka nchi ya Angola, babake kutoka Sao Tome, bibi yake kwa upande wa baba alitoka nchi ya Senegal ila bibi wa babake alitoka nchi ya Brazil! Mshairi, msanii na mwalimu wa sanaa, Raquel Lima anajitokeza kwenye kitabu hiki na hata nakala ya sauti kama sehemu ya safari ya miaka kumi ya haswa ushairi simulizi, harakati ambayo imewezesha kudhuru zaidi ya nchi kumi na mboli barani Ulaya, Amerika Kusini na Afrika. Katika kipindi hiki, aliwasilisha kazi yake ya fasihi, hadithi simulizi, ushairi shindani – almaarufu poetry slam, mashairi ya spoken word, utendaji, na tafrija za muziki zinazojulikana kwa kireno kama FLIP – Festa Literária Internacional de Paraty, FLUP Rio - Festival Literário das Periferias, FOLIO – Festival Literário Internacional de Óbidos, Festival Silêncio, Palavras Andarilhas, miongoni mwa zingine. Uwezo wake wa kuchanganya aina mbalimbali za sanaa, ustadi wa kumbukumbu na jamii, uangalifu katika masuala ya kutokuwepo usawa na hata ile hamu ya kutafiti na kuelewa mizizi yake ilimfanya arudi chuoni, ambapo anaendeleza utafiti wake ukilenga usimulizi na utumwa katika visiwa yya SãoTomé na Principe katika Kituo cha Masomo ya Kijamii cha Chuo Kikuu cha Coimbra.



Shinaz ndiye Mratibu wa Tamaduni wa Feminist Republik na ana utaalamu na uzoefu mkubwa kusimamia ruzuku, ikiwa amefanya kazi UAF-Africa tangu 2013. Maarifa yake ya kina kuhusu ukweli wa wanawake wanaoishi pembezoni mwa jamii, hususan kwenye mitaa ya mabanda mijini, ikiwa ni pamoja na shauku yake ya kutumia uigizaji na densi kama vifaa vya uponyaji na utunzaji wa pamoja, ujuzi ambao ametumia kufanya kazi kote barani Afrika akibuni pamoja na watetezi wasanii katika kuinua mbinu za haki jamii ili kufanikisha maswala ya muda mrefu ya haki za wanawake na hakisheria ya kijinsia. Katika UAF-Africa, Shinaz amechukua jukumu muhimu la kupigania haki za jamii zilizotengwa, watetezi wa haki za kimazingira na watetezi - wasanii wa kifeministi.
Shinaz anapatikana kwenye mitandao ya Instagram: @nubianqueenbiz_zaids na on LinkedIn: Shinaz Rehema Ali



Sr. Letta Mosue ni mmoja wa watoto 9 (wa kike 8 na wa kiume 1). Alipofika umri wa miaka 14, wazazi wake wote wawili walifariki na akajiunga na kanisa ilikuwa mtawa. Aliweza kukamilisha masomo yake ya shule na kusoma masomo ya chuo kupitia njia ya barua. Alifanya kazi kama mwalimu kwa miaka 11 na kuhudumu kama mwalimu mkuu kwa muda wa mwaka mmoja katika shule moja ya kati mjini Pretoria. Alijisajili kusomea saikolojia. Mtawa Letta alitoka kwenye familia ya waponyaji ingawa alilelewa kwney imani ya Kikatoliki, familia yake walifanya Uponyaji wa Kiasili wa Kiafrika. Kanisa lilipinga matendo haya na shangazi yake alitishwa kwamba atafurushwa kanisana iwapo angeendelea. Alijua kwamba alikuwa na kipaji cha uponyaji wakati ambapo alikuwa akisomea shahada ya uzamili, yaani Master's degree ya saikolojia ya kliniki. Hili lilizua uhasidi mwingi sana, lakini, lakini kulikuwa na mtawa mwenzake ambaye pia alikuwa na kipaji kama hicho na ambaye alikuwa mshauri wake. Alikitetea kipaji hicho na anaendelea kufanya uponyaji wa Kiafrika na saikolojia hadi wa leo. Amesalia pia kwenye uongozi katika usharika wake wa Watawa.

# Utambulisho wa Waliochangia



Dk. Toyin Ajao (Mungu wa kike) anachukua ulimwengu kama msomi wa umma, mwanaharakati wa wanawake, mtafiti wa jumla wa mambo, mwandishi wa hadithi na mwandishi. Yeye ndiye Mwanzilishi wa Kituo cha iAfrika cha Utafiti wa jumla na Praxis; kulenga mabadiliko ya kibinafsi na ya kibinadamu (uponyaji) kupitia matokeo ya msingi na nguvu ya upendeleo wa kitaifa. Alipokea MA katika Migogoro, Usalama na Maendeleo kutoka Chuo cha King's London na uhasibu wa BSc kutoka Chuo Kikuu cha Obafemi Awolowo, Ile-Ife. Anashikilia PhD katika Sayansi ya Kisiasa kutoka Chuo Kikuu cha Pretoria, ambapo hapo awali alikuwa mhadhiri wa Mahusiano ya Kimataifa. Ajao ni Mshirika wa Utafiti, alumna na mratibu wa sasa wa Kituo cha Uongozi wa Afrika (ALC). Yeye pia ni mfadhili wa zamani wa daktari wa Next Gen-SSRC, Andrew Melon Foundation na ALC.

Barua pepe: teeajao@yahoo.com



Zanele Mbugua ni mwanaharakati wa kifeministi Mkenya ambaye an shauku kuhusu utetezi wa haki za wanawake, akilenga haswa haki za watu wa LBTQI+ na pia haki za afya ya uzazi na ngono. Ana shahada ya Bachelor of Arts kwenye somo la Saikolojia kutoka Chuo Kikuu cha Rhodes (Afrika Kusini). Kwa sasa Zanele anasomea Shahada ya Uzamili katika somo la Jinsia na Maendeleo katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Kama Bingwa wa Feminist Republik, Zanele anatazamia kuchangia kujengwa kwa ajenda ya Feminist Republik yenye nguvu na inayohakikisha wanawake nan a watu wasioambatana na jinsia yoyote kupata ulinzi kamilifu na usalama, ustawi na haki ya uponyaji. Unaweza kuwasiliana na Zanele kupitia Instagram: @zane_ee na

LinkedIn: Zanele Mbugua



Melissa Wainaina ni mfeministi Mwafrika anayeishi nchini Kenya. Anahusika kikamilifu katika nafasi za kifeministi za Kiafrika ambazo huendeleza ulinzi wa jumla na usalama wa wanawake na watu wasiojiambatanisha na jinsia yoyote, pamoja na utunzaji wa pamoja na ustawi, haki ya uponyaji na mipango ya uandishi wa nyaraka zinazoshawishiwa na ufeministi. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 12 katika sekta mashirika ya kijamii, ambapo amefanya kazi tangu 2006 akilenga zaidi ujinsia, haki za kijinsia na za kujamiiana. Melissa ana uzoefu mkubwa katika kuimarisha uwezo wa njia zinazotegemea haki katika kazi ya mabadiliko ya kijamii. Melissa ndiye Mwezeshaji wa Ubunifu wa Feminist Republik na Mhariri Mku wa jarida la Dzuwa.



Solome Nakaweesi ni mwanaharakati wa kifeministi kote Afrika, mshiriki kikamilifu na mchambuzi katika harakati za haki za wanawake, haki za binadamu, haki za kijinsia nchini Uganda, Afrika na Kimataifa. Amehusika kwa karibu sana katika kusaidia kuibuka (na kufufua) harakati za kisasa za kijamii na mashirika katika bara la Afrika, Kanda ndogo ya Afrika Mashariki na nchini Uganda. Solome ni mwezeshaji mashuhuri na mtaalam wa kujitunza mwenyewe kibinafsi, ustawi na haki ya uponyaji na amepitia uzoefu wa safari ya kibinafsi na PIA ile ya pamoja na watetezi wengine wa haki za binadamu. Solome ndiye Mhariri Mgeni wa Toleo hili la kwanza na Dzuwa.



# DZUWA

**Dzuwa ni chapisho huru la hariri lililoletwa kwako na Feminist Republik , inayojulikana kama Jukwaa la Watetezi Wanawake wa Haki za Binadamu wa Afrika**

**Imefadhiliwa na Urgent Action Fund -Afrika kama jukwa lililojawa na hadithi chungu nzima, kushiriki na kujifunza; jukwa hili ni la  watetezi haki wakina wanawake, wabadili jinsia na wasio ambatana na jinsia kujielimisha kwa mambo ya usalama, uponyaji na ustawi yao binafsi na jamii yao ...**


**Barua Pepe:**
**feministrepublik@uaf-africa.org**


**Pata hapa wito wetu maluum ya misaada  ya pesa ya kuboresha mikakati ya kuibunisha hali ya uponyaji na ustawi ya jamii**


**July 2020**

The Feminist Republik